BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,021,208,577/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Maajabu** ya panya Kennedy mrithi wa panya Magawa

UKURASA 3



# Nipashe

Alhamisi Agosti 11, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581034
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
ram.com/theguardian_newspaper

## UCHAGUZI KENYA

# Odinga, Ruto jino kwa jino

**Maofisa** saba wa tume wafutwa kazi, mgombea anaswa na silaha...

*Endelea ukurasa 2*



Raila Odinga    William Ruto

UKURASA 22

## WERNER AREJEA RASMI RB LEIPZIG KUTOKA CHELSEA

UKURASA WA 5

## WANAWAKE WAONGOZA MARADHI YA MOYO

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imesema katika kipindi cha siku 39 kilichoanzia mwaka wa fedha 2022/23...

UKURASA WA 5

## MAJERUHI WATANO AJALI ILIYOUA 20 WAHAMISHIWA HOSPITALI BUGANDO

MAJERUHI watano kati ya 15 waliopata ajali iliyoua watu 20, wamepewa rufani kwenda Hospitali ya Shinyanga na Bugando...



Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Awadhi Juma Haji (wa tatu kushoto), akionesha baadhi ya chupa za vilevi zilizokutwa ndani ya gari dogo aina ya Toyota IST lililopata ajali ya kugonga trekta eneo la Mwakata wilayani Kahama, walipotembelea eneo la tukio juzi jioni. Kushoto ni Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa. **Habari Uk wa 5. PICHA: SHABAN NJIA**

# Serikali yatinga shule ya mazingira hatarishi

UKURASA 4



## Samia aagiza kujengwa kituo cha malezi ya watoto sokoni

UKURASA 2

**MICHEZO** BINGWA SUPER CUP KUBEBA BILIONI 233/- UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia aagiza soko kujengwa kituo cha watoto

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, kutenga eneo la soko kuu la mkoa huo kwa ajili ya huduma maalum ya chumba cha kulea watoto wa chekechea wakati mama zao wakiendelea na biashara.

Akizindua soko hilo lenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 10, Rais Samia alishuhudia kinamama wakiendelea na biashara huku wakiwa wamebeba watoto wao mgongoni.

"Nimetembelea soko, lakini nimeona kinamama wakiwa wamebeba watoto mgongoni, itakuwa vizuri wakamegewa sehemu wakaweka eneo la kuangalia watoto wao kwa maana hiyo wakati mama yupo kazini na biashara zake, watoto wanashughulikiwa mahala pazuri, wanapata chakula vizuri, wanakua vizuri, wanapata elimu huku wanatunzwa vizuri kwa hiyo mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya katika soko hili angalieni nafasi nzuri muiweke vizuri kwa ajili ya watoto," aliagiza.

"Badala ya mama kukaa na mtoto mgongoni kutwa nzima itamletea matatizo ya mgongo hapo baadaye. Kwa maana hiyo watoto wawe wanatunzwa sehemu moja ili na nyinyi muwe mnafanya kazi zenu," alisema.

Alisema azma ya serikali ni kuwaweka wafanyabiashara pamoja kutoka kwenye jina la wamachinga watu wanaotembea tembea hadi kuwa wafanyabiashara rasmi.

"Serikali yenu itaendelea kujenga masoko ya aina hii ya ukubwa mbalimbali katika miji mbalimbali ili wafanyabiashara, wananchi wa Tanzania wapate huduma mahali pazuri," alisema Rais Samia.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa ngazi zote kuacha kujikweza na badala yake kuwahudumia wananchi kwa kusikiliza kero na kuzitafutia ufumbuzi.

Aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa hadhara katika viwanja vya Sabasaba mjini hapo kuwa utawala bora unaenda sambamba na kuhudumia wananchi.

"Viongozi wa mkoa hadi chini niwaombe sana tuhudumie wananchi tutumikie wananchi sisi sio watawala, sisi ni wahudumu tunatoa huduma kwa wananchi, unapita unasikia kero nyingi za wananchi kama kweli tutafanya kazi tukahudumia wananchi haya makero yaliyobakia madogo madogo. Unamkuta mzee anatoka huko analia anapiga kelele katikati ya watu, ukiwatuma maofisa kamuulizeni kero, mwingine ana kibango akikionyesha mmekidaka mmekificha," alisema.

"Niombe sana muende mkahudumie wananchi tumewekwa na Mungu ametuteua tuhudumie wananchi, twendeni tuhudumie wananchi na tuwahudumie kwa utawala bora, kama umebahatika kukaa hapo ulipokaa mwananchi akija msikilize vizuri, msikilize na uchukue hatua shida yake aliyokuja nayo, tukifanya hivyo taifa letu tutalijenga kwa umoja na mshikamano, wananchi hawa hawana shida, shida yao ni kutumikiwa," alisema.

"Tunapokwenda kuwaomba kura, tukisha kukaa kwenye viti tunawageuka hiyo nimewasikia wananchi ndiyo maana nawaambia viongozi wenzangu twendeni tukahudumie wananchi," alisema.

Akijibu ombi la Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Jassel Mwamwala, kuomba Njombe kuwa manispaa, Rais Samia alisema kwa sasa serikali imezuia kukata maeneo yote ya utawala kwa sababu kufanya hivyo ni kuongeza gharama za uendeshaji na kwamba hivi sasa mwelekeo ni kwa wananchi.

"Mwelekeo ni mapinduzi ya kilimo, mwelekeo ni kunyanyua hali ya uchumi kwanza kabla hatujakatiana maeneo ya utawala, kwa hiyo hili naomba nilitolee jawabu hilo," alisema.

Alisema mikoa ya Nyanda za Juu Kusini itaingia kwenye awamu ya pili ya filamu ya 'Hidden Tanzania' kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyofichika.

Naye mlezi wa mkoa wa Njombe, Dk. Frank Hawadhi, ambaye ni mchumi wa CCM alisema, serikali inatekeleza ilani kwa vitendo na kwamba ifikapo 2025 mambo yote yatakuwa yamekamilika.

Kwa upande wake, Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, amepiga marufuku mawakala kuchakachua mbolea ya ruzuku ya serikali itakayoanza kusambazwa nchini kote ifikapo Agosti 15, mwaka huu.

Bashe aliwaonya mawakala kutothubutu kuingia mkenge wakutishwa na watu wenye fedha watakapokuwa wanauza mbolea ya ruzuku kwa bei halali iliyotangazwa na serikali na kujitokeza watu wenye pesa kuwataka wauze bei wanayoona ina faida kwao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, alimshukuru Rais Samia na kumwahidi kupandisha uchumi wa wananchi.




Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (wa saba kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Dastan Kamanzi (watatu kulia), wakiwa pamoja na waandishi wa habari wa IPP Media, baada ya kufunga mafunzo kuhusu uandishi wa habari wa data, yaliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Utawala wa TGL, Rehema Songoro. **PICHA: JOHN BADI**

# Odinga, Ruto jino kwa jino uchaguzi

**Na Maulid Mmbaga**

WAGOMBEA wawili nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya, Naibu Rais William Ruto wa Chama cha United Democratic Alliance (UDA) na Raila Odinga, wanachuana vikali katika matokeo yanayoendelea kutangazwa na Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo.

Kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi, waliojitokeza kupiga kura wanakadiriwa kuwa karibu asilimia 60 ya waliojiandikisha, idadi ambayo ni ndogo kulinganishwa na asilimia 80 katika uchaguzi uliopita. Katika mchuano huo mkali, wawili hao jana walikuwa wakipishana kwa kura chache kwa kila mmoja akiongoza kwa muda na kisha kuangushwa kulingana na kila matokeo yanapotangazwa kutoka katika vituo vya kura kwenye maeneo mbalimbali.

Kwa mfano, matokeo hayo yalionyesha idadi ya kura na asilimia kwenye mabano, majira ya saa saba mchana Raila Odinga alikuwa na kura 2,377,537 (asilimia 51.55), Ruto 2,170,817 (asilimia 47.08), Wajackoyah 19,501 (asilimia 0.42) na Waihiga 8,840 (asilimia 0.19).

Ilipotimu majira ya saa 10 jioni, matokeo yalikuwa Odinga 2,403,304 (asilimia 51.74) na Ruto 2,178,897 na ilipotimu saa 11 jioni Odinga 2,408,438 (asilimia 51.75) na Ruto 2,182,446 (asilimia 46.9).

**UTATA WAIBUKA**

Wakati matokeo hayo yakiendelea kutangazwa, utata uliibuka baada ya baadhi ya kaunti kushindwa kupiga kura ya magavana kutokana na tatizo la usahihi wa majina na data.

Vyama vya kisiasa nchini humo vilipinga uamuzi wa Tume ya Uchaguzi (IEBC) kusitisha upigaji kura katika nafasi nne ya uchaguzi katika Kaunti ya Mombasa na Kakamega.

Miungano miwili mikuu ya Azimio One Kenya unaoongozwa na Odinga na United Democratic Alliance ulio chini ya Ruto, ilikitishwa na uamuzi huo, ikidai kuna hila na ufisadi katika mpango huo mzima.

Maofisa wa chama wanahofu hitilafu hiyo inaweza kuathiri matokeo ya uchaguzi. Pia iliripotiwa kuwa mamlaka ya uchaguzi ilisimamisha uchaguzi wa ugavana kaunti za Mombasa na Kakamega baada ya karatasi za kura kubainika kuwa na makosa ikiwamo maelezo na picha za wagombea kutokuwa sahihi.

Katibu Mkuu wa Muungano wa Azimio One Kenya, Junet Mohamed, alisema amesikitishwa na hatua hiyo, akidai kuna mpango wa siri kwa kuwa maeneo yaliyoathiriwa wanayazingatia kama ngome yao.

"Sisi hatujafurahishwa na hatua ya kamati ya uchaguzi kuahirisha uchaguzi wa ugavana katika kaunti ya Mombasa na Kakamega, tunaona kama kuna mpango wa siri, ambao bado tunachunguza kwanini ni hizo kaunti mbili ambayo ni ngome ya Azimio peke yake uchaguzi umeahirishwa na sio kaunti zingine," alisema Junet.

Mgombea wa ugavana wa UDA, Hassan Omar, alisema yeye na mgombea mwenza wake walishtushwa na taarifa za kuahirisha uchaguzi wa ugavana wa Mombasa.

"Ninaona kuna njama mbaya katika uahirishaji huu uliyokusudiwa," Hassan alidai.

Aliongeza kuwa timu yake inajadiliana na mamlaka ya chama na kwamba kauli rasmi itatolewa kuhusiana na suala hilo.

IEBC ilitetea uamuzi wake, ikisema dosari hiyo haikutokana nao, akisisitiza kampuni iliyopewa kandarasi ya kuchapisha karatasi za kupiga kura ndiyo ilichanganya karatasi hizo.

Alisema kampuni imeanza uchapishaji wa karatasi za kupigia kura na hivi karibuni watatangaza tarehe ya uchaguzi katika maeneo hayo.

Katika hatua nyingine, tume hiyo imewafuta kazi wafanyakazi saba baada ya kudaiwa kukutwa wakiwa nyumbani kwa mgombeaji kwa kile kinachoaminika kutaka kushawishi matokeo ya uchaguzi huo.

Kulingana na TaifaLeo, aliyekuwa Gavana wa Nairobi, Mike Sonko, alifukuzwa na maofisa wa polisi kutoka kituo cha kupigia kura baada ya makabiliano na Gavana wa Mombasa, Ali Hassan Joho.

Hii ilitajwa kuwa ni baada ya video kuibuka ikimwonyesha Sonko akisukumwa kwenye kiti cha nyuma cha gari lake huku akizingirwa na maofisa wake wa usalama.

Gazeti la People Daily, liliripoti kuwa mgombea wa ubunge wa Ikolomani kupitia Amani National Congress (ANC), alikamatwa baada ya kupatikana na silaha hatari katika kituo cha kupigia kura.

Mpaka sasa utaratibu wa kuhesabu kura unaendelea Kenya, huku ikielezwa kuwa Tume ya Uchaguzi itatangaza matokeo mchana baada ya kukamilisha kuhesabu kura.

# Panya Kennedy kumrithi Magawa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

BAADA ya Panya Magawa kufariki dunia mwanzoni mwa mwaka huu, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro, kimempata mrithi wake mwenye jina la Kennedy ambaye ataendeleza majukumu aliyokuwa akifanya Magawa.

Hayo yalisemwa jana na Msaidizi wa utafiti Kitengo cha Apopo, SUA, Dk. Said Mshana kuwa Kenendy anafanya vizuri kazi na ameongezewa majukunu.

"Kwa kifupi panya Kenendy anaendelea vizuri na majukumu yake ya kila siku ambapo tumemuongezea majukumu zaidi ikiwamo utafutaji wa binadamu wakati wa majanga jambo ambalo litaleta tija sana kwa taifa letu," alisema Mshana.

Alisema kuwa zoezi la utafutaji binadamu wakati wa majanga mafunzo kwa panya huyo linaendelea kwa kufungiwa kamera mgongoni ambayo itakuwa ikionesha matukio yote yanayoendelea ikiwa ni pamoja na kunasa sauti za waathirika wa tukio.

Dk. Mshana alisema, wakati panya huyo akiendelea na majumu yake, kuna watu watakuwa wananasa sauti na kupata taarifa za watakaokuwa wakihitaji msaada hali itakayosaidia kukamilisha zoezi zima la uokoaji.

Alisema Kennedy pia amebobea kusaidia watu wenye majanga hasa nyumba zilizobomoka kwa kubeba kamera kama binadamu kisha kurekodi matukio.

Dk. Mshana alisema kuwa matukio yote hususan yaliyopo ndani ya nyumba ambayo imeanguka itakuwa rahisi kwa Jeshi la Zimamoto na uokoaji kufanya shughuli za uokozi kwa kuwa panya huyo atakuwa akirekodi kila kitu kitachokuwa kikiendelea huku watu walioko nje wakipokea taarifa.

Aidha, alisema panya huyo amefundishwa kugundua vimelea vya kifua kikuu na kutegua mabomu ardhini na kwamba wapo waliotumwa nje ya nchini kama Zimbabwe, Msumbiji na Kambodia kwa ajili ya kutegua mabomu ardhini kutokana na nchi hizo kuathiriwa zaidi ili ardhi itumike kwa kilimo.

Wananchi wa Mkoa wa Morogoro wameshukuru kazi za utafiti mbalimbali zinazofanywa na chuo hicho na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano unapotakiwa hasa chuo kitakapokuwa kikihitaji panya kwa ajili ya mafunzo.

Mrefu Shaban, mkazi wa Morogoro alisema, Chuo cha SUA kina kila sababu ya kupongezwa kwa kugeuza wanyama na wadudu waharibifu kuwa fursa na Watanzania wana kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopo chuoni hapo.

# Madereva mtandaoni walia gharama kupanda mafuta

**Na Halfani Chusi**

BAADHI ya madereva wa usafiri mtandaoni wamelalamika kupanda kwa bei ya mafuta kunavyoathiri biashara yao huku wakiomba Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kuboresha tozo za nauli ili ziendane na hali halisi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jijini Dar es Salaam, walisema baadhi yao wameamua kuachana na huduma hiyo baada ya kupiga hesabu na kugundua faida inayopatikana haikidhi mahitaji, tofauti na ilivyokuwa awali.

Jumanne Juma, dereva bajaji anayetumia mtandao wa BOLT, alisema ameacha kutumia mtandao huo kwa muda wa siku tatu kutokana na kutopanda kwa bei elekezi tangu mafuta yalipopanda.

"Leo nina siku ya tatu situmii BOLT, kwa sababu kwenye mfumo huo kuna bei elekezi na bei haijaongezwa, lakini mafuta yameongezeka sasa ikifika jioni ukipiga hesabu unakuwa umefanya kazi ya mafuta tu, na ukifanya masihala hata hesabu ya bosi unaweza kukosa, kwahiyo hili ongezeko la mafuta limetuathiri sana, faida hamna kabisa na kazi imekuwa ngumu sana," alilalamika.

Abilah Masudi, dereva wa gari anayetumia mtandao wa PING, alisema kampuni nyingi zinaangalia maslahi binafsi na kushindwa kuongeza bei wakihofia kukosa wateja.

"Tatizo kweli bei ya mafuta ipo juu, lakini wamiliki wa kampuni walio wengi wanajiangalia wenyewe kwa kiasi kikubwa wengi wao wanafahamu bei ya mafuta imepanda, lakini kuongeza bei ya usafiri kwenye mtandao hawataki wakihofia kukosa wateja sasa ukiangalia hali ya mafuta mwisho wa kazi unaona hakuna ulichofanya.

"Kama jana nimeshuka na laki moja, lakini katika laki hiyo nimetumia mafuta ya Sh. 60,000 bado hapo nakatwa hela kama tozo ya mtandao asilimia 20, kwa hiyo nikajikuta nabakiwa na 20,000 bado gari inahitaji huduma kwa hiyo ukiangalia sasa hivi hali ilivyo ni tofauti na mwanzo, angalau mwanzoni ulikuwa unaweza kubakiwa hata na 50,000 baada ya kutoa mafuta na makato ya huduma," alifafanua.

Dereva wa Bodaboda, Peter Chuwa, anayetumia Mtandao wa Moon, alisema ongezeko la bei ya mafuta limemfanya ashindwe kuendelea kutumia mtandao huo kwa sababu tangu bei ya mafuta ipande hajapata faida katika kazi yake, huku akiiomba serikali kuangalia uwezekano wa kushusha bei ya mafuta.

"Dah! Hili suala la mafuta kupanda kwa kweli limeturudisha nyuma sana kama mimi nimeshindwa kabisa kuendelea na kazi kutokana na hasara niliyokuwa napata kila siku, kwahiyo naiomba serikali ifanye iliangalie," alisema.

"Vijana wengi watakosa kazi kwa sababu wengi tunaoendesha hivi vyombo vya usafiri sio vya kwetu ni vya mabosi wetu kwahiyo ukishindwa kazi inabidi urudishe chombo kwa bosi na unabaki mtaani," alisema.

Kwa upande wake dereva bajaji anayetumia mtandao wa Litoride, Alima Malenda, alibainisha kuelemewa na ugumu wa kazi akilinganisha na awali kabla ya mafuta kupanda bei.

"Sisi tunaotumia mtandao kupata abiria kwa kipindi hiki tupo katika wakati mgumu sana yaani ukiweka mafuta ya Sh. 20,000 kwenye bajaji unaweza kupata Sh. 50,000 hapo ukitoa pesa ya bosi, bando, pamoja na hela ya kuhudumia bajaji unajikuta unabaki na Sh. 2,000 ya kurudi nayo nyumbani," alisema na kuongeza:

"Hili suala limefanya baadhi yetu wengi waache kutumia mtandao kupata abiria na wengine wamaeacha kazi kabisa hata mimi nakomaa kwa sababu sina kazi nyingine ya kufanya," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

LATRA

## TAARIFA KWA UMMA

### MIKUTANO YA KUKUSANYA MAONI KUHUSU VIWANGO VYA NAULI ZA TRENI KWA MIKOA YA DAR ES SALAAM, KIGOMA NA MWANZA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) ikiomba ongezeko la nauli kwa asilimia 15 kwa abiria wanaotumia usafiri wa treni Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria Na. 3 ya LATRA, 2019 Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kuridhia viwango vya nauli kwa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ikiwemo nauli za treni.

Katika kulitekeleza hilo, Mamlaka imeandaa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa usafirishaji, ikiwa ni pamoja na watoa huduma, watumiaji wa huduma na wananchi kwa ujumla.
Mikutano hiyo itafanyika tarehe 19, 22 na 24 Agosti 2022, kwa Dar es salaam (Ukumbi wa Anatorglo) Kigoma (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) na Mwanza (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) mtawalia.

**Nauli zinazopendekezwa na TRC ni Kama ifuatavyo:**

Jedwali Na. 1. Nauli za treni ya abiria ya 'Deluxe' kutoka Dar es salaam

| Vituo | Umbali | Daraja la pili-kulala | | Daraja la pili-kukaa | | Daraja la tatu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Km | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa |
| Ruvu | 79 | 13,800 | 15,800 | 8,300 | 9,500 | 5,800 | 6,700 |
| Wami | 151 | 18,000 | 20,700 | 10,800 | 12,400 | 7,600 | 8,700 |
| Morogoro | 202 | 21,200 | 24,300 | 12,700 | 14,600 | 8,900 | 10,300 |
| Mkalamo | 203 | 21,200 | 24,300 | 12,700 | 14,600 | 8,900 | 10,300 |
| Kilosa | 289 | 25,400 | 29,200 | 15,300 | 17,500 | 10,700 | 12,300 |
| Korogwe | 291 | 25,400 | 29,200 | 15,300 | 17,500 | 10,700 | 12,300 |
| Mombo | 335 | 27,500 | 31,600 | 16,500 | 19,000 | 11,600 | 13,300 |
| Dodoma | 465 | 34,900 | 40,100 | 21,000 | 24,100 | 14,700 | 16,900 |
| Same | 459 | 33,800 | 38,900 | 20,300 | 23,400 | 14,200 | 16,400 |
| Moshi | 558 | 39,100 | 45,000 | 23,500 | 27,000 | 16,500 | 18,900 |
| Arusha | 644 | 44,400 | 51,000 | 26,700 | 30,600 | 18,700 | 21,500 |
| Tabora | 850 | 54,900 | 63,200 | 33,000 | 37,900 | 23,100 | 26,600 |
| Urambo | 940 | 59,200 | 68,000 | 35,500 | 40,800 | 24,900 | 28,600 |
| Kigoma | 1,254 | 76,100 | 87,500 | 45,700 | 52,500 | 32,000 | 36,800 |

Jedwali Na. 2. Nauli za treni ya abiria daraja kawaida kutoka Dar es salaam

| Vituo | Umbali KM | Daraja la Kwanza | | Daraja la Pili | | Daraja la Tatu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli zamani | Nauli Pendekezwa |
| Pugu | 20 | 12,200 | 14,000 | 10,600 | 12,100 | 6,100 | 7,000 |
| Ngerengere | 144 | 20,700 | 23,800 | 16,600 | 19,100 | 9,000 | 10,300 |
| Morogoro | 202 | 24,300 | 28,000 | 19,200 | 22,000 | 10,200 | 11,800 |
| Kimamba | 271 | 28,000 | 32,200 | 21,700 | 25,000 | 11,500 | 13,200 |
| Kilosa | 289 | 29,200 | 33,600 | 22,600 | 26,000 | 11,900 | 13,700 |
| Dodoma | 465 | 40,100 | 46,100 | 30,300 | 34,900 | 15,600 | 18,000 |
| Manyoni | 595 | 47,400 | 54,500 | 35,500 | 40,800 | 18,100 | 20,800 |
| Itigi | 635 | 49,800 | 57,300 | 37,200 | 42,800 | 18,900 | 21,800 |
| Tabora | 850 | 63,200 | 72,600 | 46,700 | 53,700 | 23,500 | 27,000 |
| Kaliua | 973 | 70,500 | 81,000 | 51,800 | 59,600 | 26,000 | 29,900 |
| Isaka | 982 | 71,700 | 82,400 | 52,700 | 60,600 | 26,400 | 30,300 |
| Uvinza | 1,141 | 81,400 | 93,600 | 59,600 | 68,500 | 29,700 | 34,100 |
| Shinyanga | 1,045 | 75,300 | 86,600 | 55,300 | 63,600 | 27,600 | 31,800 |
| Mto Ugalla | 1,083 | 77,700 | 89,400 | 57,000 | 65,500 | 28,500 | 32,700 |
| Katumba | 1,149 | 81,400 | 93,600 | 59,600 | 68,500 | 29,700 | 34,100 |
| Mpanda | 1,183 | 83,800 | 96,400 | 61,300 | 70,500 | 30,500 | 35,100 |
| Mwanza | 1,229 | 86,200 | 99,200 | 63,000 | 72,500 | 31,400 | 36,000 |
| Kigoma | 1,254 | 87,500 | 100,600 | 63,900 | 73,500 | 31,800 | 36,500 |
| Nauli zinazopendekezwa zitawasilishwa kwa ufafanuzi zaidi wakati wa mkutano husika | | | | | | | |

Kutokana na umuhimu wa mkutano huo, LATRA inawaalika wadau wa sekta ya reli na wananchi kwa ujumla kushiriki bila kukosa katika mkutano kama ilivyoelezwa hapo juu.

LATRA pia itapokea maoni kwa maandishi. Maoni hayo yawasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, S.L.P. 3093, Dar es Salaam, iliyopo katika Jengo la Mamlaka, Barabara ya Nkrumah kabla ya **tarehe 31 Agosti, 2022.** Aidha, maoni ya wadau yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia anuani hizi: **info@latra.go.tz** na **dg@latra.go.tz .**

**Imetolewa na:**

J. J. Kahatano

**Kny: Mkurugenzi Mkuu,**
**9 Agosti, 2022**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Jengo la LATRA Makao Makuu, Mtaa wa Nkrumah 454/160, S. L. P. 3093, Dar es Salaam
Simu + 255 222 197 500/2, Nukushi: + 255 222 116 697
Barua pepe: dg@latra.go.tz , info@latra.go.tz , Tovuti: www.latra.go.tz

216984301

# Serikali yatinga shule ya mazingira hatarishi

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amezuru kwenye Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa na kuahidi serikali itajenga madarasa, nyumba za walimu na vyoo ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni hapo.

Ziara hiyo imetokana na ripoti maalum iliyotolewa na Nipashe kwa siku nne mfululizo kuanzia Jumapili iliyopita, ikieleza hali mbaya ya miundombinu ya shule hiyo, kwa maana ya nyumba za walimu, madarasa na vyoo, ambavyo ni hatari kwa usalama wa wanafunzi na walimu.

Katika ziara hiyo, Silinde alifuatana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Sinyamule na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Mpwapwa. Maofisa wa idara nyeti za serikali pia walikuwamo katika ziara hiyo.

Baada ya Silinde kuwasili shuleni hapo juzi, alikagua miundombinu ya madarasa, vyoo, nyumba za walimu na samani za shule hiyo, akikiri kuyashuhudia yaliyoripotiwa na Nipashe.

"Kweli Shule ya Kiboriani ina uhitaji wa madarasa, nyumba za walimu kwani hizi zilizopo inadaiwa zilijengwa kwa nguvu za wananchi mwaka 1987.

"Jitihada ya Mheshimiwa Rais ni kuboresha miundombinu ya elimu, katujengea madarasa na katika bajeti ya mwaka 2022/23 tumetenga Sh. bilioni 55 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu," alifafanua.

Naibu Waziri Silinde alibainisha mikakati ya kunusuru hali mbaya ya miundombinu na samani shuleni hapo kwamba Serikali Kuu itatoa fedha kwa ajili ya kujenga vyumba viwili vya madarasa na nyumba moja ya walimu itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia familia tatu (3 in 1).

Aliwaomba wananchi wa Kijiji cha Kiboriani kushiriki uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo ili kuunga mkono jitihada za serikali, akisititiza Rais Samia amedhamiria kuboresha sekta ya elimu.

"Changamoto tumeipokea, Ofisi ya Rais - TAMISEMI tutaongeza madarasa.

Ni lazima tukubali kuongeza nguvu ya kusaidia walimu maeneo ya pembezoni. Niwaombe anzisheni operesheni kuokoa walimu, sisi pia tutasaidia hata nyumba moja ya 'three in one' ambayo itahudumia familia tatu za walimu watatu.

"Wananchi na viongozi wa vijiji hatupaswi kumkatisha tamaa Mheshimiwa Rais, kwa kuwa hata ninyi mnao wajibu wa kushiriki kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo yenu.

"Niseme tu kwamba kama serikali, tuna mipango mbalimbali ya kutatua changamoto kama hizi nchi nzima kupitia Mradi BOOST ambao una lengo la kuimarisha elimu msingi na una fedha takriban Sh. trilioni moja ambao utajenga madarasa ya shule za msingi 9,705 na kukarabati shule za msingi kongwe kwa mwaka wa fedha 2022/23," alisema.

Silinde alibainisha kuwa kupitia mradi huo, kero kama hizo zilizopo katika Shule ya Msingi Kiboriani, zitakuwa historia na bado wanaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vitakavyosaidia kumaliza kabisa kero ya miundombinu shuleni.

Alisema kuna mradi mwingine wa kuboresha elimu ya sekondari (Sequip) ambao una lengo la kujenga shule za sekondari 1,000 na shule za sayansi kwa ajili ya wasichana kwenye mikoa yote nchini. Alibainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha wameshaanza kujenga shule 224 za sekondari na shule za wasichana kwenye mikoa 10 nchini.

"Lakini tuliona tusiwekeze kwenye madarasa tu, bali pia tuboreshe mazingira ya walimu, hivyo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, tumetenga jumla ya Sh. bilioni 55 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 809 zenye uwezo wa kuchukua kaya 1,916

"Hivyo, siyo kwamba serikali hatuoni hizi changamoto au hatuzifanyii kazi, tunajitahidi kuzitatua kadri rasilimali zinavyopatikana kwa sababu tuna shule za msingi zaidi ya 17,000 na shule za sekondari zaidi ya 4,000.

"Na kati yake, nyingi ni za zamani, hivyo zinahitaji ukarabati wa mara kwa mara ilhali tunahitajika kuendelea kujenga miundombinu mipya kwa kadri ya mahitaji.

"Kutokana na changamoto niliyoiona hapa, tutaleta madarasa manne kukabiliana na upungufu, matundu ya vyoo sita pamoja na nyumba ya mwalimu yenye uwezo wa kubeba familia tatu, yaani 'three in one'," Naibu Waziri Silinde aliahidi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary, alimwahidi Naibu Waziri huyo kuwa ataendelea kuihamasisha jamii kuchangia juhudi za serikali katika kuboresha miundombinu ya shule.

"Kazi kubwa inafanywa na serikali lakini pia jamii ina wajibu wa kushiriki na kuunga mkono jitihada hizo, hivyo leo hii (juzi) nitafanya kikao na wananchi wa Kiboriani ili tuhamasishane kuendelea kuboresha shule hii ambayo ni muhimu kwa watoto wa kijiji hiki," Rosemary aliahidi.

Awali, akisoma taarifa ya Shule ya Msingi Kiboriani, Kaimu Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Mpwapwa, Agness Nkacha, alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule 122 za halmashauri hiyo na ilianza kutoa huduma mwaka 1979 na mpaka sasa ina wanafunzi 420 na walimu sita ambao wote ni wa kiume.

Katika uchunguzi wake, Nipashe ilibaini walimu walioko kazini ni watano, mwalimu mwingine hajarejea kazini kwa takriban mwaka mmoja sasa kutokana na kile kilichoelezwa na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Satiel Kasanda, kwamba mtumishi huyo alipata ajali ya pikipiki wakati akipanda mlima kwenda kazini, hivyo ni mgonjwa.

Kaimu Ofisa Elimu Agness alibainisha kuwa Shule ya Msingi Kiboriani ipo umbali wa takriban kilometa 20 kutoka makao makuu ya wilaya na inakabiliwa na upungufu wa madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo.

Alisema katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, serikali imepanga kujenga vyumba viwili vya madarasa kwa Sh. milioni 40 na matundu sita ya vyoo kwa Sh. milioni 6.6 ili kukabili uhaba huo.

**MKAKATI WILAYANI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, George Fuime, akizungumza na Nipashe jana wilayani hapa kuhusu ziara ya Naibu Waziri Silinde shuleni Kiboriani, alisema wana mpango kuunda timu ambayo wataitumia kufanya ukarabati wa shule zote ambazo zipo katika hali mbaya wilayani hapa.

Alisema kuwa katika kikao kijacho cha Baraza la Madiwani, atakutana na Kamati ya Fedha ili kujadiliana namna watakavyotenga fungu maalum kwa ajili ya kufanya ukarabati katika shule zote ambazo ziko katika hali mbaya kimiundombinu na samani.

"Kuna shule zina hali mbaya kuliko hii ya Kiboriani, haya majengo ukilinganisha na zile shule, bado unayaona ni mazuri kabisa. Zipo shule kama Malolo hali yake ni mbaya sana.

"Hivyo, hatuwezi kuendelea kujenga madarasa mapya tu kila siku, lazima tuwe na timu ya ukarabati tutakayoitumia kila inapohitajika," alisema Fuime ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mpwapwa Mjini inakopatikana Shule ya Msingi Kiboriani.

Akizungumzia mikakati yao kuinusuru Shule ya Msingi Kiboriani, Fuime alisema halmashauri ilikuwa na taarifa za uchakavu wake, hata kabla ya kuripotiwa na Nipashe, lakini walikubaliana kuanza na ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kiboriani na baadaye wahamie kwenye uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo.

"Tulikubalina kuanza na zahanati ya kijiji ambayo kila kaya inatoa Sh. 20,000 kwa ajili ya kuchangia ujenzi. Niliona jana kwenye taarifa za serikali kwamba serikali italeta Sh. milioni 50 ili kumalizia zahanati.

"Tulipanga baada ya kumaliza ujenzi wa zahanati, tuanze kukarabati shule hii na kwa fedha ambazo zimetengwa katika bajeti hii ya Sh. milioni 40 tutahakikisha tunajenga madarasa mawili pamoja na ofisi ya walimu.

"Baadaye kuna nyumba ambayo tulishaanza mchakato wa ujenzi kwa kushirikiana na wananchi, pia tutakwenda kuijenga ili kuongeza idadi ya nyumba kutoka ile ya 'three in one' ambayo Naibu Waziri Silinde ameahidi ili walimu wote sita wapate nyumba nzuri," Fuime aliahidi.

Katika uchunguzi wake, Nipashe ilibaini shule hiyo haina ofisi kwa ajili ya walimu na ilipohoji kwa Mwalimu Mkuu Kasanda, alibainisha kuwa kuna chumba kidogo katikati ya madarasa, ndicho ofisi yake na kwamba walimu wenzake shuleni hapo hawana ofisi.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, David Silinde (aliyenyoosha mkono), alipozuru katika Shule ya Msingi Kiboriani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**"Kweli Shule ya Kiboriani ina uhitaji wa madarasa, nyumba za walimu kwani hizi zilizopo inadaiwa zilijengwa kwa nguvu za wananchi mwaka 1987.**

HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini waungana kuhamasisha sensa

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

VIONGOZI wa dini katika Halmashauri ya Mlimba, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro, wameungana na Kamisaa wa Sensa nchini, Anne Makinda, kuwasihi wananchi kujitokeza kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi, iliyopangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Viongozi hao kutoka madhehebu mbalimbali ya dini walisema hayo wakati wakizungumza na vyombo mbalimbali vya habari katika halmashauri hiyo, kwenye zoezi lililokwenda sambamba na harambee ya ujenzi wa kanisa la Moravian Mlimba na kushauri wenzao kutumia nyumba za ibada kufikisha elimu juu ya umuhimu wa sensa.

Baadhi ya viongozi hao, Mchungaji Esau Wihadile wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Ulanga, alisema zipo faida nyingi kwa wananchi kuhesabiwa ni jukumu la viongozi wengine wa dini kuhimiza na kusisitiza jambo hilo hasa kwa kutumia kila ibada wanazofanya.

"Kwanza tunaunga mkono kauli ya kamisaa wa sensa nchini mama Anne Makinda aliyeomba viongozi wa dini tushiriki uhamasishaji wa zoezi hili, nia ni kufanikisha malengo mahususi ya zoezi hili, hasa mipango ya serikali katika kujua idadi ya watu wake na kuona namna bora ya kuwahudumia," alisema.

Alisema viongozi wa dini kushirikishwa vyema tangu mwanzo kwenye sensa imewarahisishia kutambua vyema umuhimu wake na kuwa mabalozi wa kuhakikisha inafanikiwa vyema.

Aidha, alisema wamekuwa wakihimiza waumini kushiriki sensa hasa kwenye nyumba za ibada na kutoa elimu ya sensa kwa watendaji wao wa chini kuanzia ngazi ya kata na jumuiya mbalimbali ili elimu hiyo iweze kufika hadi ngazi za chini kabisa kwa mtu mmoja mmoja.

Kwa upande wake Mchungaji Isaya Mwanjalwa kutoka Kanisa la Moravian Mlimba, alieleza umuhimu wa kuhesabiwa na kubainisha lengo kuu la serikali ni kuhakikisha wanafahamu idadi sahihi ya watu wake ili iwe rahisi kutoa huduma na kwamba hakuna sababu ya mtu kutoshiriki kwa kuwa atawakosesha serikali taarifa muhimu za kuwasaidia wananchi hao.

Naye mratibu wa anwani za makazi kitaifa kutoka Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia, Mhandisi Jampyon Mbugi, aliwasitiza wananchi kujua vyema taarifa zao ili iwe rahisi kuzitoa wakati wa zoezi la sensa.

Alitaja baadhi ya masuala muhimu watakayopaswa kuyafahamu kurahisisha sensa ni jina, eneo analoishi sambamba na viongozi wa eneo husika.

Alisema zoezi la anwani za makazi kwenye halmashauri ya wilaya hiyo lilifanyika vyema na kwa sasa kila mwananchi anaweza kujua vyema anwani yake na kurahisisha sensa na kuwasihi wananchi kujitokeza na kuwa wazi.

# Majeruhi watano wa ajali wahamishiwa Bugando

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAJERUHI watano kati ya 15 waliopata ajali iliyoua watu 20, wamepewa rufani kwenda Hospitali ya Shinyanga na Bugando kwa matibabu zaidi.

Kati ya majeruhi hao wamo mke na mume waliovunjika sehemu mbalimbali za miili yao ikiwamo nyonga, miguu na mikono na kuhitaji matibabu zaidi ili kunusuru maisha yao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama Dk. Deogratius Nyaga, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya hali za majeruhi zinavyoendelea pamoja na miili ya watu waliofariki katika ajali hiyo ambao tayari 16 kati ya 20 wameshambuliwa na ndugu zao.

Alisema, kati ya majeruhi 15 watano wameshapata rufani kwenda katika hospitali hizo, watatu wamepelekwa Bugando, wawili Shinyanga na mmoja amechukuliwa na ndugu zake kuelekea mkoani Tabora kwa matibabu zaidi.

Dk. Nyaga, aliwataja waliopelekwa Bugando kuwa ni Mwasiti Samweli (23) alivunjika miguu yote, mikono na nyonga, Daines Haule (43), alivunjika mguu mmoja na Godfrey Kaganda (47), aliyevunjika nyonga na kuumia kichwani.

Wengine ni Omary Shabani (26) aliyechukuliwa na ndugu zake kwenda Tabora na Paul Sebastiani (44) aliyepelekwa Hospitali ya Rufani Shinyanga, aliyevunjika miguu yote miwili sehemu ya mapaja na alikuwa akilalamila kupata maumivu kifuani.

Dk. Nyaga alisema, hakuna vifo vilivyoongezeka kutokana na huduma ambazo zinaendelea kutolewa na wataalam mbalimbali hata kwa wale ambao walikuwa hawana ndugu zao walipata matibabu kupitia msamaha unatolewa hospitalini kupitia Ofisi ya Ustawi wa Jamii.

Alisema, kati ya miili ya watu 20 walioripotiwa kufariki dunia, 16 mpaka sasa imeshatambuliwa na ndugu zao na wanaendelea na kuchukuliwa kwa taratibu za mazishi na iliyosalia ndani ya siku saba ikikosa ndugu, itachukuliwa taratibu nyingine za kiserikali.

Dk. Nyaga alitaja miili iliyotambuliwa na kuchukuliwa na ndugu kuwa ni Tungu Magesa (28), Jonas Kija (49), Paul Choyo (23), Sebastiani Kimaro (28), Kano Lutemba (48), Julius Jacobo (28), Mussa Ally (25), Sarah Siti (46), Augustino Mnyamba (28), Nuhu Mpinga (27), Leonard Basu (52), Aman Dishoni (35), Nicolous Budole (34), Flora William (26), Erick Peter (26) pamoja na Salinja Pambe (25).

Mmoja wa ndugu wa majeruhi Zuberi Jafari alisema, mgonjwa wake anaendelea na matibabu vizuri na hali yake inaridhisha baada ya wataalamu kumpatia matibabu kwa haraka.

Pia, alishukuru msaada wa serikali wa kuhakikisha huduma na dawa zinapatikana kwa wakati na kuwatembelea wagojwa kujua hali zao imewatia moyo huku akisisitiza kuwa waendelee kuwa na moyo huo kwa kuwa unawapatia faraja wagonjwa kwa kuona hawajatelekezwa na serikali.

Mfamasia wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dismas Masele alisema, awali ofisi ya Mkuu wa wilaya ilikuwa na Mfuko wa Maafa ambao ikitokea ajali za dharura wanapokea wagonjwa na kutibiwa baadaye wanaandika madai kisha mfuko huo unalipa gharama zote zilizotumika kutibia majeruhi.

Alisema, kwa sasa utaratibu huo umebadilika na wanapokea wagonjwa wa dharura na kuwapatia matibabu kupitia msamaha ambao unatolewa kupitia kitengo cha Ustawi wa Jamii na wagonjwa wote 15 walipata matibabu kupitia kitengo hicho na sasa hali zao zinaendelea vyema.

**KAMANDA ATEMBELEA ENEO LA AJALI**

Kamanda wa Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbrod Mutafungwa, alitembelea eneo la ajali hiyo na kuagiza magari yote kuwa na viakisi mwanga (reflector).

Pia, alionya tabia ya madereva kutumia vilevi kabla au wakati wanaendesha magari na kusema kwenye gari la IST walikuta vinywaji vya aina mbalimbali ikiwamo chupa zilizokuwa nusu pombe.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akiwa ameushika Mwenge wa Uhuru, baada ya kukabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, katika Kijiji cha Mseko Wilaya ya Iramba, jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanawake waongoza kwa maradhi ya moyo

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imesema katika kipindi cha siku 39 kilichoanzia mwaka wa fedha 2022/23, imetoa huduma kwa wagonjwa 11,242, wanawake wakiwa 6,458.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Prof. Mohammed Janabi, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipotoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za JKCI na mwelekeo wake kwa mwaka huu wa fedha.

Prof. Janabi alisema katika kipindi hicho cha Julai hadi Agosti 8 mwaka huu, wamehudumia idadi hiyo, watu wazima wakiwa ni 9,642 na watoto ni 1,600.

"Kati ya 11,242, wanaume ni 4,784 na wanawake ni 6,458. Kliniki zetu zilitoa huduma kwa wagonjwa 10,926 na kulaza wagonjwa 316 ambapo kati yao watu wazima ni 267 na watoto ni 49 na wagonjwa watatu walipoteza maisha," alisema.

Prof. Janabi alisema JKCI inatoa huduma kwa wagonjwa kati ya 300 na 350 kwa siku kwenye kliniki na kulaza kati ya wanane na 10 kwa siku.

Alisema taasisi hiyo inafanya aina mbili za upasuaji mkubwa wa moyo ambao ni wa kupasua kifua na kutumia tundu dogo kwa kutumia mtambo wa Cathcab.

"Tunapasua kifua kati ya wagonjwa wanne na watano kwa siku na kwa kutumia tundu dogo wagonjwa kati ya 10 na 15 kwa siku. Kwa kipindi hiki wagonjwa 63 wamefanyiwa upasuaji wa kufumua kifua, mishipa ya fahamu na mapafu ambapo watu wazima ni 42 na watoto 21," alisema.

Prof. Janabi alisema kwa upande wa upasuaji mkubwa wa kutumia tundu dogo, watoto waliofanyiwa ni 12 na watu wazima 104 na kufanya jumla ya wagonjwa 117.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, taasisi hiyo ilitengewa Sh. bilioni 40.8 ambapo walitoa huduma kwa wagonjwa 117,181, wanawake wakiwa ni 58,145 na wanaume ni 59,036 kwenye kliniki ambapo kati ya hao wagonjwa 47 walitoka nje ya Tanzania.

"Kupitia fedha hizo, taasisi ililaza wagonjwa 4,195, wanaume wakiwa ni 2,237 na wanawake 1,958. Wagonjwa 512 walifanyiwa upasuaji wa kufungua kifua ambapo watu wazima walikuwa ni 265 na watoto ni 247 na upasuaji mkubwa kutumia tundu dogo walikuwa wagonjwa 1,936 ambapo kati yao watu wazima ni 1,856 na watoto 80," alisema.

Prof. Janabi alisema katika mwa huu wa fedha 2022/23, taasisi imetengewa Sh. bilioni 44.5 ambazo zitatumika kulipa mishahara, uendeshaji wa taasisi ikiwamo ununuzi wa vifaa tiba na dawa, kusomesha wafanyakazi 50 na miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi wanaochangia watoto kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya moyo kwenye mitandao ya kijamii hasa makundi ya WhatsApp, kabla ya kufanya hivyo wawasiliane na uongozi wa taasisi ili kupewa utaratibu mzuri.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ichukue hatua kwa vitendo vinavyokashfu imani

**AGOSTI 8,** mwaka huu, Klabu ya Soka ya Simba iliadhimisha tamasha maalum, maarufu kama 'Simba Day' katika Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam. Tamasha hilo, pamoja na mambo mengine, lilikuwa na lengo la kutambulisha kikosi chake kipya kwa ajili ya msimu wa Ligi Kuu ya NBC mwaka 2022/23 pamoja na michuano ya kimataifa.

Kama ilivyo ada, tamasha hilo hutanguliwa na burudani mbalimbali kama vile muziki kutoka kwa wasanii mbalimbali na ubunifu kutoka kwa mashabiki.

Sambamba na mambo hayo, tamasha hilo huhitimishwa na mechi kati ya Simba na timu iliyoalikwa mahususi kwa ajili ya kunogesha tamasha hilo na kuwapa burudani wapenzi na kuonyesha umahiri wa kikosi kipya kilichosajiliwa.

Kwa mwaka huu, Simba iliialika timu ya St. George kutoka Ethiopia na kuiadhibu kwa mabao 2-0.

Pamoja na mambo hayo, tamasha hilo liliibua taharuki baada ya msanii Tunda Man kuingia uwanjani akiwa amebebwa kwenye jeneza, kukiwa na msalaba na mtu aliyeigiza kama kiongozi wa dini ya Kikristo, aliyevaa joho na stola huku mkononi akiwa amebeba Biblia. Baada ya kufika uwanjani, aliyevaa mavazi ya kichungaji, alibainisha kwamba ndani ya sanduku hilo kuna mtu ambaye alifariki dunia Agosti 6, mwaka huu, na chanzo cha kifo chake ni maneno aliyokuwa akiyatoa.

Tarehe hiyo ambayo pia ilionyeshwa kwenye msalaba, ilikuwa siku ambayo Yanga ilikuwa na kilele cha Wiki ya Wananchi na ilicheza mechi kati yake na Vipers ya Uganda na kufungwa mabao 2-0.

Kutokana na matokeo hayo, watu hao waliingia na jeneza uwanjani, walikuwa kama wanaigiza utani kama ilivyo jadi kwa klabu hizo mbili kongwe nchini hasa baada ya Yanga kufungwa.

Licha ya kuwa ulionekana ni utani, suala hilo limeibua taharuki kwa watu mbalimbali wakiwamo baadhi ya viongozi wa dini ambao wameweka bayana kwamba suala hilo ni kejeli, dharau na unajisi dhidi ya dini ya Kikristo kwa kile kilichoelezwa kuwa kwa imani ya dini hiyo, msalaba ni ishara ya ukombozi kwa waumini wao.

Baadhi ya viongozi wa dini walikwenda mbali zaidi kwa kusema watu wanaoigiza mambo kama hayo na kufanya dhihaka mbele ya Mwenyezi Mungu, hawana mwisho mwema na kitendo hicho kinaashiria maafa katika jamii ikiwamo misiba na majanga ya asili.

Kutokana na kitendo hicho, serikali tayari imeshachukua hatua kadhaa ikiwamo kumwondoa katika nafasi yake meneja wa uwanja kwa kile kilichoelezwa kushindwa kutekeleza masuala la kiusalama katika eneo hilo.


Kwa ujumla, kitendo hicho si tu kwamba ni cha fedheha na dhihaka dhidi ya Ukristo bali kwa watu wa imani zote kwa kuwa kimeshusha na kudhalilisha heshima ya dini na hata waumini wake.

Ni vyema serikali ikachukua hatua madhubuti kudhibiti vitendo kama hivyo kwa kuwa licha ya kudhalilisha na kukashfu imani mojawapo, kinaweza kusababisha machafuko katika jamii ikiwamo kuzuka mvutano baina ya dini moja na nyingine na kusababisha maafa. Tunapaswa kujifunza katika mataifa mengine ambayo migogoro ya kidini imesababisha kuwapo kwa umwagaji wa damu dhidi ya watu wasio na hatia.

Vitendo kama hivyo vya kuigiza vimekuwa vikifanywa katika mechi baina ya Yanga na Simba pamoja na wasanii wa tamthilia mbalimbali nchini.

Ufike wakati sasa serikali ipige marufuku vitendo hivyo kwa kuwa havina mwisho mwema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Takataka barabarani zinaichafua nchi'

Na Halfani Chusi

**UGONJWA** sugu wa kushindwa kuhifadhi taka kabla hazijapelekwa dampo unaendelea kukosa tiba kwenye mikoa na miji mingi.

Hii ni kutokana na majiji na miji kupambwa na marundo ya taka pembeni ya barabara, mitaani na ndani ya mitaro.

Kwa hali hiyo kunahitajika namna bora ya kuhifadhi taka kabla hazijachukuliwa kwenda kutupwa dampo.

Kila mara kumekuwapo na mazoea ya kuacha takataka kwenye maeneo hayo zikisubiri kukusanywa na kupelekwa dampo, lakini zikikusanywa na kuwa milima ya marundo ya uchafu mijini.

Taka hizo zinaachwa kando ya barabara lakini zinatumbukia mitaroni na hata nyingine kutokana na wingi wa milima zinasambaa hadi kwenye maeneo ya makazi zikirundikana kwa miezi kadhaa kusubiri gari la taka lifike kuziondoa.

Ni jambo jema taka hizo kukusanywa kwa utaratibu unaotumika lakini madhara yake ni makubwa katika jamii hasa wakazi wa maeneo jirani.

Kuna athari kama maradhi hii ni kutokana na taka zinavyorundikwa zinasababisha wadudu wachafuzi kama panya, mende, inzi na hata nyoka wanaozalia ndani ya marundo hayo.

Aidha taka, zinanuka na kuchafua hali ya hewa, huku majimaji zikichuruzika yakichafua mazingira na kusababisha kinyaa.

Taka kuachwa hadi kutoa harufu kali na kubakiza wadudu pale chini zilipokusanywa baada ya kuondolewa ni kero nyingine kwa mazingira.

Ni chanzo cha kusababisha maradhi mbalimbali kama kipindupindu, kuhara, kutapika damu, malaria na homa ya dengu kutokana na mazalia ya mbu.

Pia, husababisha uchafuzi wa hali ya hewa kwa kiwango kikubwa kwa sababu taka hizo zinapooza zinanuka na kuacha hali hiyo kwa muda mrefu.

Wakati umefika wa kuangalia njia bora ya kutupa taka hizo na kama makandarasi wakionekana wanafanya vibaya na hawatimizi wajibu ipasavyo mikataba yao isimamishwe na wengine wenye vifaa na vitendea kazi wapewe jukumu hilo.

Serikali inapaswa kulichukulia hatua suala hili si jambo jema kuendelea kuishi na taka kwa miaka mingi na historia kuonyesha kuwa Dar es Salam na miji mingine ya Tanzania ni michafu na hiyo ni kawaida yake.

Ni vyema serikali ikatenga maeneo maalumu na yenye miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kuhifadhia taka kabla hazijachukuliwa na magari kutupwa dampo.

Kama likifanyika hilo ni matumaini yangu kuwa hakutakuwapo tena na mrundikano wa taka kando ya barabara kitu ambacho kinachafua mandhari na kushusha heshima ya taifa.

Mrundikano wa taka unasababisha kuwapo na kazi ngumu kwa magari ya taka ambayo yanajaa shehena za taka barabarani na hata kukera watumiaji wengine.

Ni vyema barabara ikabaki na suala moja tu la kupitisha vyombo vya moto na siyo kugeuzwa maghala ya taka.

Takataka barabarani ni maua yanayoonekana zaidi majiji ya Dar es Salaam, kuanzia kwenye barabara kuu na barabara za mitaa kama maeneo ya Mwananyamala kwa Mama Zakaria, kwa Kopa na kuelekea barabara ya Kinondoni.

Maeneo hayo imekuwa kama utamaduni kurundika taka kando ya barabara hadi zinaoza na kuwa kero zaidi wakati wa mvua.

Nimetumia ukurasa huu adhimu kufikisha kilio cha wanajamii wengi ili serikali, wizara na mamlaka za afya kuangalia namna bora ya kuzihifadhi taka kabla hazijachukuliwa kwenda kutupwa dampo.

Unahitajika usasa zaidi kwenye kutunza taka na kutengeneza utaratibu ambao Watanzania wataachana na mazoea ya kukerwa na takataka kila wakati.

HABARI KITAIFA

# Madeni chanzo vyombo vya habari kuyumba

**Na Jenifer Gilla**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limesema vyombo vya habari binafsi, mpaka sasa vinazidai taasisi za serikali zaidi ya Sh. bilioni 7.8 kutokana na matangazo yaliyotolewa katika vyombo hivyo.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema hayo jana Dar es Salaam alipozungumza na Radio One huku akibainisha kwamba tatizo hilo limesababisha baadhi ya vyombo vya habari kuyumba kutokana na kukosa pesa za kujiendesha kwa kuwa pesa nyingi ziko nje. Balile alisema hilo ni moja ya mambo yanayosababisha watilie mkazo mabadiliko ya sheria ya habari, ili kuzibana taasisi ambazo hazilipi madeni hayo.

"Vyombo vya habari binafsi vinadai taasisi za serikali zaidi ya Sh. bilioni 7.8 na hawalipi kwa kuwa hakuna msukumo wa kufanya hivyo. Msukumo wa mabadiliko hayo ni kuweka sheria ya kuwafunga pale watakaposhindwa kulipa.

"Agosti 11 na 12, mwaka huu, katika mkutano wa wadau wa habari, hatuendi kushikana mashati na serikali bali tunakwenda kupigania maslahi ya wanahabari na vyombo vyao," alisema Balile.

Mwenyekiti huyo alisema vyombo vya habari kama ilivyo uwekezaji katika maeneo mengine, vinahitaji mtaji na biashara kubwa ni matangazo kwa hiyo taasisi zinaposhindwa kulipa pesa hizo kwa wakati, zinakwamisha katika uendeshwaji.

"Hapo kuna mishahara ya waandishi, wafanyakazi wa idara zingine kwenye vyombo vya habari, kuna fedha za uchapaji, lakini matumizi ya ofisi. Fedha hizi zisipolipwa, ofisi zitaendeshwaje?" alisema Balile.

Alisema jambo hilo alishamweleza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kutoa maelekezo kwa taasisi hizo kulipa madeni hayo lakini hazijatekeleza.

"Sasa kwenye mkutano huo, mambo kama haya tutazungumzia ndiyo maana tunataka kuwe na sheria za namna hii ili kulinda maslahi ya waandishi na uhai wa vyombo vya habari nchini," alisema.

Balile alisema wanahabari wamekuwa wakiwajibika kwa namna utaratibu unavyoelekeza na ndio maana vyombo vya habari vinatumika kupeperusha matangazo, lakini wajibu wa baadhi ya taasisi hautekelezwi.

"Sasa katika mabadiliko haya, suala la malipo ya matangazo liwekwe kisheria, atakayekaidi ajue kwamba ipo sheria na atawajibika kwa hayo," alisema.

Balile pia alisema TEF na wadau wa habari wanasisitiza uhuru wa vyombo vya habari katika kujisimamia kama zilivyo tasnia zingine nchini tofauti na sasa mkurugenzi wa habari ndiye amebeba jukumu hilo.

"Yaani huku mkurugenzi wa habari anakuwa mlalamikaji, msikilizaji na hakimu. Hapo huwezi kutendewa haki. Tunataka kuwapo na Baraza Huru la Vyombo vya Habari ambalo serikali ikiwa na jambo lake au imekwazwa iende huko badala ya wao walalamike, wasikilize na kuhukumu," alisema.




Ofisa Mkuu wa Wateja wa Jumla wa Benki ya NMB, Alfred Shao (kushoto), akichangia mada kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa fedha na haki katika mamlaka, wakati wa kongamano la Nishati, jijini Dar es Salaam lililowakutanisha wadau wa sekta ya mafuta na gesi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima kicheko ruzuku bei mbolea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imeweka wazi bei ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima itakavyokuwa huku wadau wakiipongeza na kushauri kuangalia bei kwa zile zinazozalishwa na kampuni zingine ikiwamo YARA.

Akizungumzia jana kuhusu hatua hiyo, Mwenyekiti wa Wakulima wa Alizeti, Stephen Marealle, alisema hatua hiyo italeta tija kwenye kilimo. "Haijawahi kutokea kuwapo na ruzuku ya bei. Kweli Rais (Samia Suluhu Hassan) anafanya kazi na tuzidi kumwombea. Lakini tunaomba mtufikishie salamu bei za mbolea za YARA hatujasikia wakulima wanaomba YARA pia bei baada ya ruzuku kutolewa zitangazwe," alisema.

Mkulima Iddi Mindi alisema kupunguza kwa nusu ya bei mbolea ya aina hizo itabadilisha kilimo nchini na itaongeza matumizi ya mbolea.

"Juzi nilinunua kilo 50 kwa Sh. 140,000 mbolea YARA. Kwa bei hizi zilizotolewa leo inaonesha jinsi gani serikali imeanza kumjali mkulima," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa bei zilizotangazwa kwa mbolea za YARA anashauri pia serikali ipitie bei za mbolea zote zinazozalishwa ndani ya nchi na zinazoagizwa kutoka nje.

"Wakulima wengi bado ni wadogo halafu hatuna elimu ya kutosha ya matumizi ya mbolea. Hatua hii ya serikali ni ya kupongezwa kama mnavyojua hali za wakulima. Kwa sasa nikienda kununua mbolea badala ya kuondoka na mfuko mmoja wa kilo 50 sasa naondoka na mifuko miwili," alisema.

Jana TFRA kupitia Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka hiyo, Dk. Stephan Ngailo, alisema serikali imepanga na kutenga Sh. bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea ili kuwapunguzia makali ya bei.

"Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza wakulima kuanza kununua mbolea kwa bei ya ruzuku ifikapo Agosti 15, mwaka huu, na wastani wa bei ya mbolea katika mpango utakuwa hivi," alisema.

Dk. Ngailo alisema kwa mbolea ya DAP, bei ya ruzuku itakuwa kwa mfuko kilo 50, Sh.70, 000 baada ya kutoa ruzuku ya serikali ya Sh.61, 676 na UREA Sh.70,000 baada ya kutoa ruzuku ya Sh.54,734.

"Aina ya CAN Sh.60,000 baada ya kutoa ruzuku ya Sh.48,156, aina ya SA Sh.50,000 baada ya kutoa ruzuku Sh.32,852 na aina ya NPKs Sh.70,000 baada ya kutoa ruzuku Sh.52,695," alisema.

Pia alisema usajili wa wakulima kwa ajili ya kunufaika na ruzuku iliyotolewa na serikali unaendelea nchini.

## Asilimia 70 wachanja UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

ASILIMIA 70 ya wakazi wa mkoa wa Ruvuma wamepata chanjo ya UVIKO-19, wakati wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchanja kwa manufaa yao.

Kampeni hiyo iliyofanyika katika Uwanja wa Majimaji mjini Songea iliendeshwa kwa kaulimbiu ya 'Mziki Mnene Ujanja Kuchanja', imewaleta wengi kuelewa umuhimu wa chanjo na kuchanja.

Akizungumza wakati wa tamasha hilo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Louis Chomboko, alisema wamevuka lengo la kitaifa kwa kuwafikia wananchi wengi zaidi.

"Lengo la taifa ni kutoa chanjo ya UVIKO-19 kwa wananchi kwa asilimia 70 kabla ya mwisho wa 2022. Hatua tuliyofikia ni mafanikio makubwa kwa kuwa tunapakana na nchi jirani hali inayosababisha mwingiliano wa watu, hivyo kuchanja ni muhimu," alisema.

"Nachukua fursa hii kushukuru Wizara ya Afya, viongozi wa kitaifa, USAID pamoja na wadau wetu FHI 360 kupitia mradi wa EpiC kwa kuhakikisha kuwa inapatikana muda wote, lakini zaidi ni kwa kutoa elimu na kuhamasisha jamii yetu juu ya umuhimu wa kupata chanjo ya UVIKO-19," aliongeza.

Alisema nguvu kubwa kwenye kampeni hiyo ni kuhakikisha kila mwananchi anayestahili kupata chanjo anaipata kwa ukaribu kwenye hospitali, vituo vya afya na maeneo mengine yaliyoruhusiwa kufuata taratibu bila usumbufu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, aliwapongeza viongozi wa afya mkoani humo kwa kuweka nguvu na kufanikisha lengo la taifa la kutoa chanjo.

"Kwa kuwa mkoa wa kwanza kufikisha lengo hili la taifa, inaonyesha ni kwa jinsi gani mmejitolea kusaidia wananchi wetu. Kwa kutumia njia zenu wenyewe kufikisha lengo na sasa kwa kutumia tamasha hili la muziki ambalo limeweza kuvuta umati mkubwa wa wananchi, nina uhakika mtaendelea kufanya vizuri zaidi," alisema.

EpiC ni mradi wa kimataifa wa miaka mitano unaotekelezwa na Shirika la FHI360 kwa ufadhili wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) pamoja na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), uliojikita kufikia na kuendeleza udhibiti wa janga la VVU/UKIMWI.

## Naibu Spika ahimiza ushiriki wa sensa

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu, amewaomba Watanzania na viongozi kuungana na Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha kujitokeza kushiriki Sensa ya Watu na Makazi ili wananchi wapate maendeleo.

Zungu alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipopokea matembezi ya Chama cha Skauti Wilaya ya Ilala waliyoanzia Buguruni hadi Viwanja vya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujitokeza katika sensa.

Alisema serikali inapojua idadi ya Watanzania, inakuwa na uamuzi sahihi wa kupanga maendeleo ya Tanzania, hivyo ni muhimu kwa wananchi kujitokeza.

Zungu alisema endapo mtu hatajitokeza katika sensa, anakosesha maendeleo katika eneo husika jambo ambalo siyo vizuri katika nchi.

"Tuungane na Rais wetu, viongozi tukubali kuhesabiwa, huwezi kupata maendeleo bila idadi ya watu kujulikana, tuendelee kuwahamasisha wananchi ili wajue umuhimu wa sensa na wajitokeze.

"'Wananchi' Klabu ya Yanga wameleta jezi kutokana na idadi ya wanachama wao na Klabu ya Simba 'mnyama' nayo imeleta jezi kutokana na idadi ya wanachama, hivyo Klabu ya Yanga itafanya kampeni ya sensa, Simba na Azam FC nao watafanya kampeni na vilabu vyote vya michezo nchini vitashirikiana kufanya kampeni ya sensa," alisema.

Zungu alisema skauti imekuwa ikifanya mambo mengi nchini, hivyo ni wakati mafaka kwao kuwa mstari mbele katika kufanya uhamasishaji wa sensa.

Alisema kero zao amezipokea na atakwenda kuzifanyia kazi ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi. Zungu aliwataka wawe watu wa kutegemewa na siyo kutegemea misaada kwa kuwa ipo mikopo ya halmashauri ambayo inaweza kuwasaidia vijana hao kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Big Bon, Mohamed Bahashwan, alisema lengo lao kubwa ni kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi katika sensa ili wapate maendeleo.

Alisema haiwezekani kupatikana maendeleo kama nchi haitakuwa na idadi ya wananchi wake, hivyo ni jukumu la kila mmoja kujitokeza Agosti 23, mwaka huu, ili kuhesabiwa.

Kamishna wa Skauti Wilaya ya Ilala, Fatuma Kalembo, alisema wanakabiliwa na shida ya usafiri katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na vifaa vya ofisi.



Waumini wa dhehebu la Shia, wakiwa katika maandamano ya Siku ya Ashura, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni kumbukizi ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammad (SAW) Imam Hussein kilichotokea huko Karbalaa Iraq katika karne ya 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hakuna kulala ujenzi bwawa la Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2,115, umefikia asilimia 67 na kwamba kuanzia sasa kazi hiyo itafanyika usiku na mchana.

Makamba alieleza hayo juzi mbele ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wahariri na wanahabari wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea mradi huo.

"Kasi kubwa ya ujenzi inaendelea katika mradi huu. Sasa hivi kazi inafanyika saa 24 usiku na mchana. Mtakuwa mashahidi leo ikiwa ni Sikukuu ya Nanenane lakini watu wapo kazini na wanabadilisha zamu tu," alisema Makamba.

Sababu nyingine kwa mujibu wa Makamba ni maboresho na mabadiliko yaliyofanyika katika menejimenti ya TANESCO pamoja na bodi yake ambazo zimekuwa zikifuatilia ujenzi wa bwawa hilo na kuwasimamia makandarasi kwa ukaribu.

"Ukitazama maendeleo ya mradi, miaka miwili na nusu ya mwanzo toka Desemba 2018 mpaka Juni, mwaka jana, tulifikia asilimia 37. Leo tuko asilimia 67 (ongezeko la takriban mara mbili chini ya mwaka mmoja). Ni kasi kubwa katika kipindi kifupi," alisema.

Katika ziara hiyo, wahariri na wanahabari walipata fursa ya kujionea maeneo manane muhimu katika mradi huo ikiwamo ujenzi wa tuta kuu ambalo Juni, mwaka jana ulikuwa asilimia 26 lakini hadi hivi sasa umefikia asilimia 78.

Maeneo mengine ni daraja la kudumu ambalo ni muhimu kupitisha vifaa vya ujenzi vyenye uzito mkubwa, ujenzi wake Juni 2021 ulikuwa asilimia 37.8, hivi sasa asilimia 95.

Pia walijionea njia za maji kuendesha mitambo ambazo ujenzi wake kuanzia Juni, mwaka jana, ulikuwa asilimia 43 lakini sasa hivi uko asilimia 85. Jengo la mitambo (power house) lilikuwa asilimia 29 na sasa asilimia 51 wakati kituo cha kusafirishia umeme (switchyard) hadi Juni 2021 kilikuwa asilimia 38 na sasa asilimia 89.7.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema: "tulikuwa tunasikia tu mradi unaendelea lakini hatukuwa na taarifa sahihi lakini leo (juzi), tumeona. Tunashukuru na kupongeza hatua iliyofikiwa kwenye mradi huu," alisema.

Bwawa la Nyerere linajengwa katika maporomoka ya Mto Rufiji mkoa wa Pwani na linatarajiwa kuzalisha megawati 2115 zitakazoingizwa kwenye gridi ya taifa ili kuongeza, kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

# Kiwanda kuanza uzalishaji mwezi ujao

**Na Mary Geofrey,** LUSHOTO

UZALISHAJI wa chai katika kiwanda cha Mponde, Lushoto, mkoani Tanga, unatarajia kuanza rasmi mwezi ujao.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, wakati akizungumza wakati wa kumpokea Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, aliyeanza ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi.

Mgumba alisema mpango uliopo ni kuanza majaribio mwezi ujao na kuanza uzalishaji baada ya kuzinduliwa Desemba, mwaka huu, lakini ametaka waanze uzalishaji wakati wa majaribio ili kuruhusu wananchi wanaovuna chai ianze kuchakatwa kiwandani hapo.

"Majaribio ya uzalishaji chai yanatarajiwa kuanza mwezi wa tisa, baada ya wiki tatu kutoka sasa kwa miezi mitatu na mwezi wa 12 kizunduliwe na kuanza uzalishaji. Lakini mimi nimekataa kama kiwanda kinaanza majaribio mwezi wa tisa uzalishaji uanze mwezi huo huo," alisema Mgumba.

Alisema alikataa kwa sababu wananchi wa Halmashauri ya Bumbuli walipatiwa mkopo kutoka benki ya NMB zaidi ya Sh. milioni 120 ambazo wamenunulia mbolea na kuweka kwenye mashamba na mwezi ujao wanatarajia kuanza kuvuna.

Kama uzalishaji hautaanza mwezi ujao, alisema chai itaoza na itakuwa hasara kwa wakulima na kuwapa deni ambalo litasababishwa na serikali.

"Mimi nitalipigania lakini wewe upo juu yangu zaidi, nawe tusaidie kulisukuma hili kwenye wizara husika inayoongozwa na Profesa Joyce Ndalichako ili kiwanda kianze kufanya kazi, kisisimame na kianze kupokea chai ya wakulima ili kuhakikisha wasipate hasara," alisema.

Naye Chongolo aliahidi kusimamia jambo hilo na kumlinda mkuu wa mkoa huo, katika kuhakikisha kiwanda kinaanza kazi mwezi ujao.

"Hivi si kuna watu hapa wamekopa mbolea, si kuna ambao wameanza kukatakata chai naziona hapa! Si mwezi mmoja tutakuwa na chai ya kuchuma? Tutaipeleka wapi, tukamwage! Hapana mwezi wa tisa kiwanda kikifunguliwa kianze kupokea na kuchakata chai za wananchi.

"Mwezi wa 12 iwe ni kuzindua kwa kukata utepe na huku wananchi wakiendelea kunywa chai na sio vinginevyo. Haiwezekani kila siku tunaenda mbele tunarudi nyuma, ndio maana nimekuja," alisisitiza Chongolo.

Chongolo alisema anamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan, majukumu pamoja na watendaji wengine aliowaamini hivyo kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake.

"Na mimi nitakuwa wa mwisho kuacha uzembe kuendelea kutukwamisha kwenye mambo,tutamshauri mwenye mamlaka (Rais Samia) kuchukua hatua ili tuachane naye tusonge mbele kwa kuwa tuko Watanzania wengi wenye dhamira ya kumsaidia Rais Samia kwenda mbele kwa kasi, wale watakaotukwamisha, wala haitakuwa gharama kuwashusha," alisema.

Kiwanda hicho kilifungwa mwaka 2013 baada ya mwekezaji Umoja wa Wakulima wa Chai Usambara (UTEGA) kukiuka masharti ya ubinafsishaji na serikali kujiridhisha pasipo shaka kwamba hakuwa na mpango wala nia ya dhati ya kukiendeleza.

Mwaka 2021 serikali iliruhusu rasmi kiwanda kuanza shughuli za uzalishaji, timu ya wataalam ilianza kuboresha mitambo ya kiwanda hicho ili kianze uzalishaji haraka huku wakiwa na mkakati wa kujenga kiwanda kipya katika eneo hilo.

# Serikali yafichua siri vijana kushindwa usaili wa kazi

**Na Joseph Mwendapole**

SEKRETARIETI ya Ajira, imesema moja ya changamoto kwa vijana wengi kukosa ajira ni kushindwa kujiandaa vizuri kabla ya kwenda kwenye usaili wa kazi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu wa Sekretarieti ya Ajira anayesimamia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Samwel Tanguye, wakati akizungumza na wanafunzi waliosoma nje ya nchi.

Wanafunzi zaidi ya 400 waliosoma nje ya nchi kwa mwamvuli wa Global Education Link (GEL), wanatarajiwa kushiriki mahafali yao, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Alisema wanapoitwa kwenye usaili wa kazi wanapaswa kujiandaa vya kutosha kwa kuhakikisha wanamudu kujibu maswali yote watakayoulizwa badala ya kukurupuka.

"Mfano umeitwa kwenye usaili wa udaktari hata kama umemaliza leo kuna mambo mengi unapaswa kujikumbusha kabla ya kwenda kwenye mahojiano, kwa hiyo unapaswa kuendelea kujifunza ili ukiulizwa jambo kwenye taaluma yako uwe vizuri," alisema.

Alisema vijana wengi wanadhani kwamba ajira zinatolewa kwa upendeleo jambo ambalo sio kweli kwa sababu zinatangazwa kwa uwazi na usaili unafanywa kwa haki kwa kila anayewasilisha maombi.

Alisema mara kadhaa sekretarieti hiyo inapoitisha usaili mkoani Dodoma, vijana wengi wa Dar es Salaam hawaendi kwa visingizio vya kukosa nauli.

Alitaja tatizo lingine kuwa vijana wengi kushindwa kusoma vizuri matangazo ya ajira na kujaza fomu za maombi ambazo hazijakamilika hali inayosababisha malalamiko kuwa ajira zinatolewa kwa upendeleo.

"Mfano umeambiwa ambatanisha cheti kilichothibitishwa na mwanasheria wewe unachukua cheti chako tu unatuma hivyo hivyo bila kupeleka kwa mwanasheria unatarajia nini wakati umeshindwa kufuata maelekezo," alisema.

Alitaja tatizo lingine vijana kukosa kazi ni kupeleka maombi ya kazi sehemu isiyohusika jambo linalosababishwa na kukosa utulivu wakati wa kusoma matangazo ya ajira.

"Unakuta nafasi za kazi zimetoka TRA, lakini aliyetangaza nafasi hizo ni Sekretarieti ya Ajira sasa mhitimu anajaza mambo yake vizuri, lakini badala ya kutuma maombi yake kwa sekretarieti iliyotangaza kazi yeye anatuma maombi hayo TRA," alisema.

Alisema, baada ya kuhitimu wanatakiwa kupeleka vyeti vyao Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuthibitisha uhalali wa cheti kwa kupitia mhusika uthibitisho.

Alisema ni kweli serikali imekuwa mwajiri mkuu, lakini hata hivyo haiwezi kuajiri Watanzania wote, wengine wanaweza kutumia ujuzi walioupata kujiajiri na kuajiri wenzao.

"Yapo mataifa kama China vijana wao wanauza ujuzi wao nyinyi tayari mnaujuzi msikae vijiweni kulalamika tumieni ujuzi wenu kutazama fursa zilizoko Afrika Mashariki, Afrika, Ulaya na hata Marekani," alisema.

Alisema milango ya uwekezaji imefunguliwa na wawekezaji wanamiminika kuwekeza kwenye miradi mbalimbali na vijana wanapaswa kujiandaa kuchangamkia fursa za kufanyakazi kwenye kampuni hizo.

Alisema vijana wengi wanaposoma wanapata ulemavu wa fikra kwamba ni lazima afanyie kazi taaluma aliyosomea hata kama anaona fursa kwenye eneo lingine zitakazomwingizia fedha nyingi.

"Unakuta msomi mzuri wa utawala wa biashara anasubiri aajiriwe ofisini, anakaa nyumbani mwaka ukimuuliza vipi anakwambia kazi hazijatoka wakati amezungukwa na fursa nyingi sana," alisema.

Aidha, alisema vijana waliosoma nje ya nchi wameona mambo mengi mazuri wanayoweza kufanya na kuwaingizia kipato tofauti na ambao hawakupata fursa hiyo.

"Nyinyi mnapaswa mtengeneze fursa za ajira kwa wengine kwasababu vichwa vyenu vimejaa ujuzi mwingi na mmeona fursa nyingi huko mlikotoka. Kukariri kwamba umesomea kitu fulani na huwezi kufanya biashara nyingine huo ni ulemavu," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi hao kwa kufanikiwa kuhitimu shahada zao nje ya nchi na kwamba ana matumaini makubwa wamepata ujuzi ambao watautumia kwa ajili ya manufaa ya kuendeleza taifa lao.

## Wavamizi eneo la DDC waamuriwa kuondoka

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka wavamizi wa eneo la ekari 1,931 mali ya Shirika la Uchumi na Maendeleo Dar es Salaam (DDC), eneo la Mwabepande mkoani Dar es Salaam kuanzia leo waanze kuondoka.

Wakati Makalla akitangaza hilo hivi karibuni, kumeshuhudiwa maeneo mbalimbali mkoani humo kukiendelea bomoabomoa kwa nyumba za wananchi wanaodaiwa kufanya uvamizi.

Akizungumza na viongozi wa DDC jana jijini Dar es Salaam, Makalla aliahidi kuwa maeneo yote yaliyovamiwa atahakikisha yanarejeshwa kuanzia leo.

"Tumetoka katika hodhi, tumekwenda katika uchumi tulio nao sasa. Je, tuna rasilimali hizi zitafanya kazi katika mfumo wa zamani au wa sasa, mawazo yenu ya bodi ni kutubadilisha.

"Agizo langu la kwanza kwenu ni kuendelea kufuatilia mali zote za DDC zirudi mikononi mwa DDC, hili ninalianza kesho (leo) (jana) nimekuja kuchokonoa, kesho ninakwenda Mwabapande kurejesha hekari 1,931, ninawarejeshea nyie." Alisema.

Makalla alisema kazi ya kuzirejesha mali za DDC zinaanza leo kwa kuanzia Mwabepande na kuwataka wale waliovamia waanze kuondoka.

"Nyie (DDC) ndio mtaniambia mnaweka vitega uchumi au basi tuwarejeshee ili mpate mtaji. Viwanja vile vipimwe mpate mtaji mwendelee mtaniambia, lakini ninakwenda kurejesha. Mtaniambia turasimishe ili mpate fedha kwenye ekari 1,931 kupata mataji muwekeze mtasema, ila kila kipande kilichoitwa DDC kitarejeshwa," alisema.

Makalla alitoa agizo la pili kwa Bodi ya Wakurugenzi ya DDC kuhakikisha inaandaa mpango mkakati wa biashara wa shirika hilo na kumpatia ili kumshawishi Rais Samia Suluhu Hassan.



Mkurugenzi wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel (kulia), akizungumza na wahitimu wa vyuo vikuu nje ya nchi, jijini Dar es Salaam jana, baada ya maofisa wa Sekretarieti ya Ajira kuwapatia mafunzo ya namna ya kupata ajira kwa urahisi. Wahitimu hao, wanatarajiwa kushiriki kwenye mahafali yao Agosti 21, mwaka huu, Mlimani City mkoani humo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## RC, NDC kutangaza kongani viwanda Kibaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, amekutana na uongozi wa Shirika la Maendelo la Taifa (NDC) kwa mazungumzo ya kuitangaza Kongani ya Viwanda inayomilikiwa na shirika hilo lililopo mjini Kibaha.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika kwenye ofisi za Mkuu wa Mkoa Kibaha juzi, Kunenge alimshauri Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Dk. Nicolaus Shombe, kuhakikisha ofisi yake inaandaa mchoro wa eneo hilo kwa ajili ya kulitangaza na kuleta wawekezaji.

"Ni wajibu wangu kuzisemea taasisi zote zilizoko mkoani kwangu, hivyo mnapaswa kuandaa mchoro ili tuweze kulitangaza kwa wawekezaji wanaotafuta maeneo ya uwekezaji," alisema Kunenge.

Akifafanua faida za uwekezaji, Kunenge alisema kuwa unasaidia kufanikisha malengo ya mkakati mkubwa wa mkoa wa kuongeza vyanzo vya mapato na eneo hilo la NDC ni muhimu na litasaidia kuongeza mapato kama atalisemea vizuri na likapata wawekezaji.

Aliwapongeza watendaji wote wa sekretarieti ya mkoa na halmashauri zote za Mkoa wa Pwani kwa utendaji kazi na kuwezesha mkoa kushika nafasi ya tatu nchini kwa kigezo cha makusanyo mengi yanayotokana na mapato ya ndani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa NDC, Dk. Shombe, alimshukuru Mkuu wa Mkoa huo kwa kukutana na ujumbe huo na kufanya mazungumzo ya kuendeleza eneo hilo.

Dk. Shombe alibainisha kuwa Kongano la Viwanda TAMCO Kibaha, lina eneo ukubwa wa ekari 201.63 na limeteuliwa kujenga viwanda katika makundi matatu ambayo ni vya dawa na vifaa tiba, kuunganisha magari na mitambo pamoja na viwanda vya nguo.

Kwa mujibu wa Dk. Shombe, eneo hilo linahitaji miundombinu ya barabara kilomita 4.8 na tayari kilomita 1.6 imeshajengwa.

Pia, alisema tayari eneo hilo limepelekewa umeme wa Kv 33 na TANESCO huku miundombinu ya maji ikiwa inaendelea kuboreshwa.

# Serikali kukagua NGO zinazohudumia vijana

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali inafanya uhakiki wa asasi zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za jamii (NGO), ili kujiridhisha kama kuna miongoni mwa zinazofanya kazi tofauti na masharti ya usajili.

Katambi alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akifungua kongamano la vijana Tanzania lililolenga kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi Agosti 23, mwaka huu.

Katambi alisema baadhi ya NGO zinaomba usajili wa kufanya kazi ya kuhudumia vijana lakini baada ya kufanikiwa, hufanya kazi zilizo nje ya masharti ziliyopewa.

"Mpaka sasa tuna NGO zaidi ya 3,000 zilizosajiliwa na asilimia 60 zinajihusisha na masuala ya kutoa huduma za vijana kwenye maeneo mbalimbali. Lakini changamoto tuliyo nayo ni kwamba baadhi hazitekelezi masharti ya usajili.

"Unakuta NGO inapata mabilioni ya pesa kwa ajili ya kutoa huduma ambayo iko kwenye masharti ya usajili, lakini badala ya kufanya kazi hiyo, mtu anaichukua anakwenda kujenga ghorofa. Kwa hiyo tumetoa agizo kwamba tukutane nazo, tuzifanyie uhakiki kwa ajili ya hatua zaidi," alisema.

Katambi aliwataka vijana wanaoaminiwa katika nafasi mbalimbali za uongozi kuhakikisha wanazitendea haki kwa kuhakikisha wanafanya kazi ya kuwahudumia wananchi na siyo kupandisha mabega.

"Niwaombe vijana wazingatie hili. Wanapopata nafasi na kuaminiwa katika uongozi, waende kuonyesha uwezo wao kwa kufanya kazi kwa bidii kuwahudumia wananchi na si kupandisha mabega kwa sababu wanapofanya hivyo wanawaharibia vijana wengine kutokuaminiwa tena," alisema Katambi.

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la NGO, Dk. Lilian Badi, alisema kauli hiyo ya serikali wameipokea na wataifanyia kazi. "Sisi kama baraza la NGO kupitia kazi zetu tunazozifanya, tuna mchango mkubwa katika maendeleo kwenye taifa hili.

"Ametuomba kwamba kazi tunazofanya ikiwamo miradi na programu tunazoziIeta za vijana zitatue changamoto zao, huu ni ujumbe muhimu sana na ninaomba wadau wote waliopo katika sekta hii ya NGO, tujitathmini na kuangali vizuri pale tunapopanga programu zetu kuhakikisha zinatatua changamoto za kundi hili," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua duka linalotembea la Kampuni ya Vodacom, mkoani Arusha juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa na Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Kaskazini, George Venanty (wapili kushoto) na Mkurugenzi wa Udhibiti wa Hatari na Utii wa Sheria wa kampuni hiyo, Agapinus Tax. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matatani tuhuma kupanga mbinu za mauaji

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi mkoani Katavi linamshikilia Machia Mbasa (65) kwa tuhuma za kula njama za kumuua Mabula Ntemange (37), chanzo kikitajwa kuwa wivu wa mapenzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Katavi, Ali Makame Hamad, alisema tukio hilo limetokea katika kijiji cha Lwafe, Wilaya ya Tanganyika, mkoani hapo.

Kamanda Makame alisema mtuhumiwa amekuwa akimtuhumu Mabula kutoka kimapenzi na mke wake mdogo pia kuchukua kodi katika vibanda vyake vya biashara vilivyoko katika kitongoji cha Lwafe wakati akiwa gerezeni kwa tuhuma za mauaji.

Alisema Polisi baada ya kupokea taarifa hizo ilichukua hatua za haraka na kufanikiwa kuzima jaribio hilo kwa kumkamata mtuhumiwa.

Makame alisema mtuhumiwa alipohojiwa alikiri kupanga njama hizo akieleza aliwakodi wauaji wawili kutoka Kaliua mkoani Tabora na baada ya kufika Mpanda walipokewa na mtuhumiwa na kuwaficha maporini wakati wakisubiri kutekeleza mauaji hayo.

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa Mbasa amekuwa akituma ujumbe wa vitisho vya mauaji kwa njia ya simu kwa watu wengine wawili wakazi wa Kijiji cha Mwamkulu, mkoani Katavi.

Kamanda alisema mtuhumiwa bado anaendelea kuhojiwa ili kubaini mtandao mzima wa watu anaoshirikiana nao kufanya mauaji na baada ya upelelezi kukamilika atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma.

**Alisema Polisi baada ya kupokea taarifa hizo ilichukua hatua za haraka na kufanikiwa kuzima jaribio hilo kwa kumkamata mtuhumiwa.**

# Bibi auawa kwa kushambuliwa na tembo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa Kijiji cha Mindu, wilayani Tunduru mkoani Ruvuma Zabibu Hussein (74), amefariki dunia baada ya kushambuliwa na tembo akiwa njiani kwenda kutembelea ndugu zake.

Tukio hilo lilitokea Agosti 8, saa nne asubuhi na kwa mujibu wa mashuhuda, wananchi walijitokeza kumwokoa bibi huyo ili mwili wake usiendelee kushambuliwa na tembo hao.

Diwani wa Kata ya Mindu, Ausi Maulidi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na tayari wametoa taarifa kwa maofisa wanaohusika na uhifadhi wa wanyamapori.

Kwa upande wake Diwani wa Viti Maalumu, Tarafa ya Matemanga, Stawa Timamu, aliiomba serikali kuwasaidia kuwahamisha wafugaji wanaokaa kwenye maeneo ya misitu ya hifadhi ili wanyama hao waharibifu wanapofukuzwa wasirudi kwenye makazi ya wananchi.

Ofisa Tarafa ya Matemanga, Emiliani Njogopa, alisema baada ya tukio hilo aliwasiliana na Askari wa Hifadhi za Jamii (VGs) Nalika ambao walienda kutoa msaada wa awali kwa kuwafukuza tembo na kutoa nafasi kwa wananchi kuchukua msiba wa ndugu yao nakuupeleka nyumbani. Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Ali, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na tayari amekwishapeleka askari wa kikosi cha idara hiyo kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao katika maeneo ya makazi ya wananchi.

Alisema hilo ni tukio la tatu kwa tembo hao kuua watu katika hali inayoonesha kutishia maisha ya wananchi wengi endapo jamii haitabadilisha tabia zao.

ama
ALHAMISI AGOSTI 11, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




**NGUVU MPYA UVIKO**
**'Tanzania iko tayari' ni kampeni inayofikisha, kuhamasisha chanjo**

Ukurasa 12




**Vijana wanapenda kulima ila...**
**Uharibifu mazingira, ukame, ukata mifuko vinawamaliza**

Ukurasa 14

# Maajabu ndani ya misitu ya hifadhi kuna panzi wa rangi nne za Bendera ya Taifa

**Na Christina Haule, MOROGORO**

TANZANIA imebarikiwa kuwa na misitu ya asili yenye vivutio vingi, lakini pamoja na kuleta mvua, kusafisha hali ya hewa na kuwa vyanzo vya maji, rasilimali hiyo sasa itatumiwa pia kuongeza pato la taifa kupitia utalii wa kiikolojia.

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Mashariki, anatangaza kuanzisha utalii ikolojia katika misitu ya hifadhi, itakayowafikisha watalii na watalaamu mbalimbali kuona na kufurahia vivutio vilivyoko ndani ya maeneo hayo.

Pamoja na kuendeleza utalii, wakala ataboresha miundombinu iliyopo, sambamba na kujenga njia mpya za kupita ili kuunga mkono juhudi za kuimarisha na kuinua sekta ya utalii zilizoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia ni mshiriki wa sinema ya Royal Tour ambayo inatangaza utalii wa Tanzania ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vingi vilivyopo nchini na kukuza uchumi.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TFS Caroline Malundo, anasema hayo kwenye maonyesho ya 46 ya Sikukuu za Wakulima Nana Nane Kanda ya Mashariki yanayofanyika kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere kwenye Manispaa ya Morogoro.

Anawataka watalii kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea maeneo yenye misitu na kujionea na kujiburudisha na vivutio vingi zikiwamo



Panzi wa taifa hapatikani kwingine ila Tanzania pekee. **PICHA:TFS**

bayoanua za kuvutia.

Anaitaja misitu ya hifadhi ya TFS kuwa ni ya Pugu Kazimzumbwi wenye safu za Kazimzumbwi, Pugu na Vikindu unaopatikana Kisarawe mkoani Pwani.

Caroline anaitaja misitu mingine ya hifadhi itakayotumiwa kwenye utalii wa kiikolojia kuwa ni hifadhi Utete ulioko Rufiji Pwani, msitu wa mazingira asilia wa Mkingu unaopatikana wilaya ya Mvomero.

Mwingine ni msitu wa hifadhi wa Kimboza uliopo wilayani Morogoro sambamba na kwamba mambo hayaishii hapo TFS itawekeza kwenye utalii wa mambo kale.

Caroline anazungumzia utalii wa magofu ya Bagamoyo na Mji Mkongwe Zanzibar ambao wageni wanazuru majengo ya kale pamoja na msitu wa mazingira asilia wa Uluguru wenye maporomoko ya Hululu.

Akizungumzia msitu wa mazingira asilia wa Uluguru uliopo katika kijiji cha Vinile kata ya Bunduki wilayani Mvomero anasema: "Katika maonyesho haya tumeandaa utalii wa ikolojia ili kumuunga mkono Rais Samia na kwamba tumeweka tangazo la kutembelea msitu huo uliobeba maporomoko ya maji ya Hululu na kupata jumla ya watalii 34 na kuwafikisha msituni."

Aidha, anawataka watalii kutembelea msitu huo wenye vivutio mbalimbali na kuwashuhudia panzi wenye rangi zote nne za bendera ya taifa yaani nyeusi, bluu, kijani na manjano.

Caroline anataja uwapo wa maua ya asili, pia kima weupe, vinyonga wa aina tatu wapo wenye pembe moja, mbili na tatu ambavyo mtalii wa ndani na nje anaweza kwenda kujionea na kujifunza kitu.

Anasema: " TFS hushughulika na kusimamia, kulinda na kuendeleza hifadhi za taifa za misitu ambazo katika maonyesho hayo wanatoa elimu kwa jamii kuhusu shughuli mbalimbali wanazofanya ikiwamo kuhifadhi misitu ya taifa na kuilinda."

Anasema yote yanafanyika kwa kufanya shughuli mbalimbali za ulinzi kama kufuga nyuki, kupanda miti katika mashamba waliyoandaliwa, kuzalisha mbegu mbalimbali za miti ambazo hutolewa kwa wana jamii na taasisi mbalimbali ili kuhifadhi mazingira.

Aidha, Caroline anaeleza kuwa wanasimamia shughuli za kilimo, uvuvi na mifugo ambayo usimamizi wake kama utasimamiwa vyema kilimo kuwa madhubuti, mifugo na uvuvi vikileta tija watajenga uchumi wa Watanzania kwa ngazi za jamii, kwa mtu mmoja mmoja na taifa lote.

"Niseme TFS moja kwa moja tunaunga mkono kauli mbiu ya maonyesho hayo inayosema 'kilimo ni biashara, tushiriki katika kuhesabiwa ili tuwe na mipango bora ya kilimo, uvuvi na mifugo endelevu.""

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TFS, anasema mafanikio yao katika hifadhi ndio yatakayoleta tija ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwa misitu ni uhai na msingi wa ustawi wa sekta zote za uchumi.

Anaikumbusha jamii kuwa watu wanapaswa kushirikikiana na sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kuleta tija kwa taifa sababu maeneo ya hifadhi ndiyo chanzo cha hali nzuri ya hewa, ndiko kwenye vyanzo vya maji, ardhi yenye rutuba, malisho ya mifugo, hifadhi ya mai ardhini kwenye ardhi oevu na maeneo ya kutunza wanyama pori na sehemu za kufuga nyuki.

Anafafanua kuwa Watanzania wakitaka kuhamia kwenye kilimo kisichotegemea mvua kutokana na nchi kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi ni lazima maji yahifadhiwe vizuri kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na hilo ndilo lengo la uhifadhi.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi Mazingira Asili ya Uluguru, Benadetha Chile, anawataka watalii kutembelea vivuto hivyo vilivyoanzishwa mwaka 2008 na kufanyiwa maboresho mwaka 2020 katika hifadhi hiyo ili kujua uzuri wa Tanzania na vivutio vyake.

Anasema idadi ya watalii inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na kwamba ni vyema pia kufanya utalii wa ndani.

Mmoja wa watalii kutoka Australia, Yasmin Yopi, akiwa Morogoro anasema yupo nchini kwa matembezi ya wiki tatu na ameamua kutembelea maporomoko ya maji ya Hululu kupitia maonyesho ya Nane Nane na kufurahia uzuri wake.

Anaeleza kuwa ameiona milima mingi, maua na maporomoko hayo na kwamba anawashauri watalii wenzake kutembelea kivutio hicho cha utalii ambacho ni bora kwa ajili ya akili na afya kwa kuwa ni tiba ya kisaikolojia.

AFYA

NGUVU MPYA UVIKO

# ‘Tanzania iko tayari’ ni kampeni inayofikisha, kuhamasisha chanjo

## • Mijini, vijijini na mikoa inayolegalega

**Na Sabato Kasika**




KAMPENI ya chanjo ya UVIKO-19 iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Julai mwaka jana, imepata nguvu na wadau wapya wanaojitokeza kuungana na serikali kuhamasisha jamii kujitokeza kuchanjwa.

Baadhi ya wadau hao ni taasisi zisizo za kiserikali, ambazo zimeungana, ili kufanya kampeni yenye lengo la kutoa elimu na kuhamasisha Watanzania kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19, iitwayo ‘Tanzania iko tayari’.

Uzinduzi wa kampeni hiyo unaoshirikisha wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za Africa Union, Access Challenge, African CDC, Jakaya Kikwete Foundation pamoja na Clouds Media Group umefanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa kampeni Ben Mcharo, anasema wanasubiri Wizara ya Afya iwapangie mikoa miwili ya kufanya kazi hasa ile ambayo wakazi wake wana mwitikio mdogo wa kupokea chanjo ili wakawahamasishe.

Mcharo anafafanua kuwa wataambatana na wataalam wa afya kutoka shirika la FH360, ambao kazi yao itakuwa ni kuchanja Watanzania watakaokuwa tayari kufanya hivyo, baada kupata elimu na kuhamasika kuchanjwa ili kujikinga na UVIKO-19.

Mratibu wa Uelimishaji na Uhamasishaji Jamii kutoka Wizara ya Afya, Peter Mabwe, aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa kampeni hiyo, anasema malengo ya kitaifa ya utoaji chanjo ni kufikia asilimia 70 ya walengwa wote ambao ni watu wa umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea ili ifikapo Desemba mwaka huu wawe wamechanjwa.

Anasema jambo la muhimu ni jamii kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kufikisha malengo ya kitaifa ya utoaji chanjo ya ugonjwa la asimia 70 ifikapo Desemba mwaka huu.

“Serikali inaunga mkono juhudi zenu wadau ambao mnajitolea kuendesha kampeni ya chanjo, ni muhimu kuendelea kuhamasiasha na kutoa elimu kwa jamii kwa kuzingatia ainisho la makundi yaliyo katika hatari zaidi kuhusu UVIKO-19, na kuona namna ya kuhakikisha ujumbe wa uelimishaji unaoandaliwa unawafikia na kuwagusa wananchi,”anasema Mabwe.

Mabwe anasema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa salama dhidi ya magonjwa na dharura mbalimbali za kiafya, na kwamba ili kufikia azma hiyo, ni muhimu wananchi wapate taarifa sahihi na kwa wakati.

“Elimu sahihi ni muhimu, ili kuepusha upotoshaji unaojitokeza kuhusu UVIKO-19 na dharura nyingine za kiafya ikiwamo wasiwasi wa hatua zinazochukuliwa kudhibiti magonjwa hayo,” anasema.

Anatoa mfano jinsi Watanzania walivyoonyesha wasiwasi kuhusu chanjo dhidi ya UVIKO-19, katika hatua za mwanzo za utoaji chanjo na kusababisha mwitikio wa matumizi ya chanjo kuwa hafifu.

“Kama ilivyo kwa nchi nyingine, Tanzania imeendelea kuhakikisha mikakati madhubuti ya kujikinga na maambukizi ya vurusi vya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na utoaji wa chanjo unatekelezwa.

Mratibu huyo anaongeza kuwa lengo ni kufanya jamii kuwa salama na kupunguza athari kwenye shughuli za maendeleo na kiuchumi nchini na duniani, ambapo anawataka Watanzania wasisite kuchanjwa.

**WALIOCHANJWA**

Hadi kufikia Julai 18 mwaka huu, watu milioni 11.4 walikuwa wamepata dozi kamili, kati ya malengo ya kuwachanja milioni 30.7 ambao serikali ilikusudia kuwafikishia chanjo hiyo.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, anayekaririwa na vyombo vya habari akisema hayo hivi karibuni na kuwataka Watanzania kuendelea kujitokeza kupata chanjo.

Waziri huyo anatoa takwimu hizo katika kikao cha viongozi wa dini wa mkoani Tanga ikiwa ni sehemu ya mkakati wa uhamasishaji wa kuongeza kasi ya kuchanja nchini.

Katika ufafanuzi wake, anasema sasa hivi imethibitika kwamba chanjo ndiyo njia pekee inayoweza kupunguza makali ya UVIKO-19 na kwamba ili kutengeneza kinga ya jamii, dunia imejiwekea malengo angalau ambayo ni kuchanja asilimia 70 ya watu wote duniani.

Anaweka wazi kuwa hali ya uchanjaji kwa mkoa huo kuwa ipo asilimia 22 kati ya asilimia 37 ya kitaifa na kwamba Wilaya ya Muheza wamechanja asilimia 69 na kufuatiwa na Pangani asilimia 40, Korogwe Mji 38, Handeni Mji 35 na Tanga jiji asilimia 26.

Idadi hiyo ya watu waliojitokeza kupata chanjo, imefikia kiasi hicho nchini ikiwa ni mwaka mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan azindue kampeni ya chanjo mwishoni mwa Julai mwaka jana.

**HOFU YA CHANJO**

Tangu chanjo ilipoingizwa nchini, kumekuwapo na dhana potofu ambazo zimekuwa zikisababisha baadhi ya watu kutojitokeza kuchanjwa wakidai kuwa chanjo ina madhara kiafya.

Miongoni mwa madhara yanayotajwa ni kifo, kuvuruga hedhi, kuharibu nguvu za uzazi kwa wanaume na wanawake na kwamba zinashambulia mfumo wa vinasaba na kuwafanya watu kuwa ‘mazombi’ ‘misukule’.

Hata hivyo, kwa mujibu wa wataalam wa afya, hoja hizo hazina mashiko, ambapo Watanzania wanatakiwa kuelimishwa na kujua ukweli kisha wajitokeze kwa wingi kuchanjwa kwa ajili ya usalama wa afya zao, pamoja na kwamba tangu mwazo serikali ilisema chanjo ni lazima.

Mabwe anawakumbusha Watanzania kuwa hoja kubwa ya upotoshaji zinatumika kuogopesha wengine au kupinga kabisa chanjo ya ugonjwa huo, na anawataka wazingetie maelekezo ya wataalam wa afya.

Anafafanua kuwa, tofauti na wale wasiochanjwa, wanaopata UVIKO-19 baada ya kuchanjwa hupata dalili za wastani zisizo na madhara makubwa ya kusababishwa kulazwa au kupoteza maisha.

MAZINGIRA

HABARI MBAYA

# Twiga, kasuku wanaelekea kwenye hatari ya kutoweka duniani

•Ni mnyama pendwa wa taifa, si yeye hata mwani unaangamia

**Na Gaudensia Mngumi**

SI jambo jema ni la kuchanganya japo wapo watakaoshangaa kuwa miongoni mwa takriban jamii 'spishi' milioni moja za viumbe hai vilivyo kwenye hatari ya kutoweka twiga na kasuku wamo.

Mnyama huyo aliyejaa kwenye hifadhi za Mikumi, Serengeti, Mkomazi na Selous yuko kwenye hatari ya kutoweka, ripoti ya Shirika la IPBES, taasisi huru ya sayansi na sera inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN) inasema.



Twiga wa Afrika Magharibi wamebakia 600 pekee.

Twiga ni mnyama wa taifa, ndege za Tanzania zina alama yake na utambulisho huo kila ndege inapofika ni picha ya twiga na maandishi 'fly the wings of Kilimanjaro'. Anapendwa akisifiwa kwa ukubwa, urefu lakini pia ni mpole si matata kama simba au chui.

"Inaweza kuwa taarifa ya kushangaza kujua kwamba hata twiga, kasuku, na miti ya mwaloni (oaks) hujumuishwa katika orodha ya aina zilizo hatarini, pamoja na 'cacti' na mwani wa pwani vinatoweka duniani."

Twiga ni wanyama pori wanaolengwa kwa ajili ya watu na watalii kula nyama yao, ngozi yao kutumika kwa urembo na mapambo. Aidha, wanakabiliwa na uharibifu wa makazi yao kutokana na kuvuna miti ili kupata kuni lakini uvunaji usio endelevu wa mkaa na ongezeko la mahitaji ya ardhi ya kilimo, ufugaji na shughuli za maendeleo.

Inakadiriwa kuwa wamebakia twiga 600 pekee wanaoitwa 'West African giraffes' waliosalia porini kwenye mapori japo wanyama hao kwa upande wa Tanzania idadi yao haikutajwa.

Twiga wa West African giraffes' ni aina au 'spishi' ya twiga wanaoitwa pia Niger au Nigerian giraffes, ni spishi ndogo inayotofautishwa na wengine kutokana na madoa au mabaka yake ya rangi nyepesi kwenye ngozi. Hawa hupatikana katika maeneo ya Sahel Afrika Magharibi.

Twiga wa Tanzania wanaitwa Maasai Girrafes au hujulikana kama 'Kilimanjaro Girraffes' ni spishi za twiga ambao asili yake ni Afrika Mashariki, hupatikana Kenya na Tanzania.

Wana madoa au mabaka tofauti na hao wa Afrika Magharibi yapo yanayofanana na nyota ambayo huanzia kwenye kwato hadi kichwani.

**MWANI MATATANI**

Mwani nao ni mojawapo ya mimea muhimu inayohitajika kwenye sayari hii na historia yake ni ya karne nyingi unaweza kuwa ulikuwa tangu miaka bilioni 1.6 iliyopita. Kwa Tanzania mwani hulimwa Zanzibar.

Huu siyo mmea wa kudharauliwa baharini una jukumu muhimu katika mazingira ya bahari kwanza ni makazi na chakula kwa viumbe hai baharini wakiwamo aina zote za samaki. Wakati una faida hiyo, jamii (spishi) kubwa kama vile 'kelp' ni vitalu vya chini ya maji vinavyohusika na makazi na malisho ya samaki baharini.

"Hata hivyo, kutumia mitambo mizito kukata na kuchimba bahari pengine ili kujenga bandari, kupanda juu joto la bahari na ujenzi wa miundombinu ya pwani kumechangia kupungua kwa viumbe hao ukiwamo mwani" inasema IPBES.

Mwani spishi ya' kelp' unaweza kutumiwa kulisha wanyama na unapoliwa unasaidia kupunguza utoaji wa gesi chafuzi zinazoharibu mazingira kwa kuwa ng'ombe , mbuzi au kondoo wakila majani hutoa hewa ukaa kwa njia ya kucheua, kinyesi na mkojo vinavyochangia kuharibu mazingira na kuongeza joto duniani.

'Kelp' aina ya mwani inaweza kulishwa kwa wanyama na inaweza kusaidia kupunguza uzalishaji wa gesi chafu.

**MITI HATARINI**

Miti mingi duniani inatishiwa kutoweka na vyanzo mbalimbali mfano, kukata magogo ya mbao, kukata miti kwa ajili ya uzalishaji viwandani, mashamba ya kilimo, kuni, mkaa , kulisha wanyama na majanga ya asili kama vile moto wa nyikani ni mambo yanayomaliza spishi mbalimbali za miti.

"Inakadiriwa kuwa asilimia 31 ya aina 430 za mialoni (oak) duniani ziko hatarini kutoweka, kulingana na orodha yenye alama nyekundu inayoandaliwa na Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) wa spishi zilizo hatarini. Na asilimia 41 iko kwenye "wasiwasi wa uhifadhi", hasa kutokana na ukataji miti kwa ajili ya kilimo na kupata mbegu za mafuta ya kupikia

Mgogoro wa sasa wa bioanuwai utazidishwa, na matokeo ya janga kwa ubinadamu, isipokuwa wanadamu wataingiliana na asili kwa njia endelevu zaidi, kulingana na wataalam wa UN.

"Ripoti ya IPBES inaweka wazi kwa uwazi kwamba viumbe wa porini kama wanyama na mimea ni chanzo cha lazima cha chakula, maeneo hayo ni muhimu kwa makazi na chanzo cha mapato kwa mamia ya mamilioni ya watu duniani kote," anasema Susan Gardner, Mkurugenzi wa Kitengo cha Mifumo ya Ikolojia katika Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP).

"Matumizi endelevu ya bioanuwai na kulinda mfumo wa ikolojia ukidumishwa utachangia ustawi wa binadamu. Lakini kuendelea kutumia rasilimali hizo bila uendelevu, hakuhatarishi tu hasara na uharibifu wa idadi ya 'spishi hizi' lakini pia tunaathiri afya na ustawi wetu na wa vizazi vijavyo."

Ripoti hiyo inasisitiza umuhimu wa watu wa 'asili' wazawa au 'indegenous' kupata haki za umiliki wa ardhi yao, kwani wameelewa kwa muda mrefu thamani ya wanyama pori na wamejifunza jinsi ya kuzitumia kwa uendelevu rasilimali zao kumudu maisha yao.

Mifano ya aina za mabadiliko ambayo yanahitajika ili kupunguza upotevu wa bayoanuwai, ni pamoja na mgawanyo sawa wa gharama na manufaa yanayopatikana na rasilimali hizo . Lakini pia yanahitajika mabadiliko kwenye maadili ya wanajamii ili kulinda na kutunza rasilimali pamoja na mifumo ya utawala bora inayotunza na kuendeleza mazingira bila woga, upendeleo wala ufisadi, UNEP inasisitiza.



Kasuku hatarini kutoweka. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MAZINGIRA

## VIJANA WANAPENDA KULIMA ILA...

# Uharibifu mazingira, ukame, ukata mifuko vinawamaliza

**Na Asia Rweyemamu**

VIJANA kutoka maeneo mbalimbali mkoa wa Kilimanjaro na Manyara wanatamani serikali na wadau kuwawezesha kiuchumi na kuwapatia elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Wanalenga kusaidiwa kujiajiri kupitia kilimo biashara ili wamudu na kuendeleza maisha yao.

Wanayasema hayo kwa nyakati tofauti wakati wa msafara maalumu wa vijana wa kuwahamasisha kushiriki katika kilimo na kilimo biashara kwa maendeleo endelevu.

Asasi ya kiraia ya Norway ya NCA na washirika wake wakiwamo viongozi wa dini mbalimbali walizindua msafara huo mwanzoni mwa mwezi huu wilayani Babati mkoa wa Manyara.

Msafara wa vijana ambao ulipita Kilimanjaro na kuhitimisha safari yake Kigoma umeambatana na wataalamu wa kilimo na ufugaji kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo na biashara pamoja na ufugaji wa kisasa kwa vijana.

Vijana wanagusia kukabiliwa na changamoto ya ajira na kutamani kujiajiri kupitia kilimo biashara lakini wanashindwa kufanya hivyo kwa sababu hawana ujuzi wala mitaji ya kuanzisha miradi na kununua pembejeo, pamoja na kugharamia kukodi mashamba.

Wanaeleza kuwa mambo mengine yanayowakwamisha kujiunga kwenye kilimo ni mabadiliko ya hali ya hewa ambayo kwa sasa ni vigumu kutabiri msimu sahihi wa mvua ili waanze kulima.

"Wengi tunatamani kujiajiri kwenye kilimo, lakini tunashindwa kukamilisha ndoto zetu kwani hatuna mtaji na taasisi za fedha hazipo tayari kutukopesha kwa sababu hatuna mali za kuweka dhamana" hayo ni maoni ya Elimariki Adayo (28) mkazi wa Kijiji cha Gademar, wilaya ya Babati huko Manyara.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Elimariki anasema, wengi hawana ardhi, hivyo ili kufanikisha kilimo biashara ni lazima kukodi ardhi ya kutosha, kuweka miundombinu ya maji pamoja na kununua pembejeo za kilimo, vyote vinahitaji fedha, wakiiomba serikali na wadau wa maendeleo kuwasaidia kwenye kilimo biashara.

"Vijana tupo tayari kujihusisha na kilimo ili tujikwamue kiuchumi lakini changamoto ni nyingi na zipo juu ya uwezo wetu, tunahitaji msaada wa serikali na wadau ili kunufaika na fursa zilizomo kwenye kilimo biashara."




Wana Babati wakishuhudia uzinduzi wa msafara wa vijana uliolenga kuhamasisha kushiriki katika kilimo na kilimo biashara. **PICHA:MWANDISHI WETU**

Lazaro Naftal (25) wa Kijiji cha Chekereni, mkoani Kilimanjaro, anasema kutokuwa na elimu ya jinsi gani wanaweza kujihusisha na kilimo biashara ni kikwazo kwao na fursa zilizomo kwenye kilimo.

"Kwa sasa tunahitaji tupatiwe wataalamu wa kilimo ambao watakuwa nasi bega kwa bega wakituelekeza namna bora ya kufanya kilimo biashara kisicho athiriwa na mabadiliko ya tabia nchi" Naftani anaeleza.

Anaongeza: "Wengi wetu tunategemea kilimo cha mvua, ambacho kwa sasa ni hasara baada ya msimu wa mvua kukata mapema kabla mazao hayajakomaa, hivyo tunahitaji sana elimu ya kilimo biashara ambacho hakitaathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa." Anasema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti vijana katika wilaya ya Hai, mkoa wa Kilimanjaro wanaelezea uhaba wa maji ni moja ya changamoto inayowakwamisha kufanya shughuli za kilimo.

"Mimi ni dereva bodaboda, elimu yangu ni ya msingi, natamani sana kujiajiri kwenye kilimo sababu naamini kwamba kitaniletea mafanikio makubwa kuliko hii kazi ninayofanya sasa", Frank Nyaki (29) mkazi wa Kwasadala Hai, anaeleza.

Aidha, anasema hana ujuzi wa kitaalamu, hivyo hategemei kuajiriwa popote, kilimo pekee ndiyo mkombozi wake lakini changamoto ya maji inamkwamisha kufika malengo.

Anatoa wito: "Tunaiomba serikali na wadau wa maendeleo waweke utaratibu maalumu wa kutambua vijana wenye mapenzi na kilimo, halafu watuwezesha ili tufike ndoto yetu ya kunufaika na fursa zilizomo kwenye kilimo biashara."

Kutoka Kijiji cha Chekereni mkoani Kilimanjaro, Daniel Mpesa (34), anaeleza kuwa fursa katika kilimo zipo nyingi ila elimu ya utambuzi wa fursa hizo ndiyo bado haijafikia wengi.

"Tunaona tuletewe makongamano mengi yanayotoa elimu za fursa zilizomo katika kilimo na namna ya kuzifikia sababu bila hivyo vijana wataendelea kulalamika hakuna ajira ilihali fursa zimewazunguka."

Katika Kanda ya Kaskazini NCA inashirikiana na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii ikiwemo kilimo.

"Tunataka tuwe na vijana wanaojihusisha na kilimo biashara kwa maendeleo endelevu ili waweze kujiajiri na kuajiri vijana wenzao" Mchungaji Andrew Munisi, Mratibu wa miradi ya kanisa Dayosisi ya Kaskazini, anasema.

Hata hivyo, pamoja na changamoto zilizotajwa lakini pia wapo vijana ambao walitoa ushuhuda jinsi ambavyo kilimo kimewakwamua kiuchumi na kutoa wito kwa wenzao wasikate tamaa.

Regnald Molel (26) Kijiji cha Nangara Babati anaeleza kuwa baada ya kukaa mtaani kwa muda mrefu bila ajira, aliamua kujihusisha na kilimo biashara kinachotumia umwagiliaji kwa matone (drip irrigation).

Anasema pamoja na mwenzake walianza kilimo biashara mwaka 2017 wakiwa na matuta mawili , sasa wanalima nyanya, mboga na mazao mengine kwenye eneo la zaidi ya ekari moja.

"Kupitia kilimo, nimejenga nyumba kubwa ya vyumba vitatu na sebule, nimenunua viwanja, nasomesha na kuhudumia familia yangu bila shida, pia mwenzangu amenunua gari la kutembelea kupitia kilimo biashara", anaeleza mafanikio alioyapata kwa hamasa.

"...tumetengeneza ajira kwa vijana wengine zaidi wapo 10, tunalishukuru sana shirika la NCA kwa kutuletea elimu ya kilimo cha umwagiliaji wa matone usioathiriwa na mabadiliko ya Hali ya hewa".

Christina Paulo (24), mkazi wa Kijiji cha Orngadida kata ya Qash wilayani Babati naye ni mmoja wa wanufaika kwa kilimo biashara kwa njia ya umwagiliaji wa matone.

Anasema: "Baada ya kupatiwa elimu nilianza na tuta moja la mboga mwaka 2009, sasa nina matuta 30, nalipa ada ya mdogo wangu anayesoma chuo pia nimenunua kiwanja".

Nizar Seleman ni Ofisa Mawasiliano na Uchechemuzi wa NCA-Tanzania, anayewataka vijana kubadili mtazamo juu ya kilimo na kujihusisha kikamilifu kwenye kilimo biashara sababu kilimo siyo adhabu bali ni fursa ya kujikwamua kiuchumi.




Vijana wa Chekereni wakieleza mambo yanayowakwamisha kilimo biashara.



## Ushirika kuingia mfumo kidigitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), inatarajia kuzindua mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika mwezi huu ambao utamrahisishia mkulima na mwanaushirika kupata taarifa sahihi za ushirika.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Benson Ndiege, akizungumza kuhusu mafanikio ya tume hiyo juzi, alisema miongoni mwa taarifa watakazopata ni maeneo ya uwekezaji, mikopo ya pembejeo na marejesho ya mkopo kwa mkulima, bei na malipo ya mazao ya mkulima.

"Taarifa za mfumo huo zitapatikana kupitia simu ya mkononi, lengo la kutekeleza jitihada hizi ni kuhakikisha vyama vya ushirika vinajiendesha kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, miongozo na taratibu zilizoko," alisema.

Pia alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23, tume hiyo itaratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuchochea maendeleo ya ushirika nchini.

Alisema pia watafanya uthamini wa mali zinazomilikiwa na vyama hivyo ili kutambua thamani halisi ya soko ya mali hizo na hivyo kuviwezesha vyama kufanya uwekezaji wenye tija.

"Tumepanga pia kuanzisha Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za SACCOS utakaotumika kama kinga ya akiba na amana za wanachama wa SACCOS ambao SACCOS zao zitashindwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama kwa kutoa mafunzo kwa maofisa ushirika 226, kukagua vyama vyote, na kuendelea kununua vitendea kazi na kununua magari kwa ajili ya kuongeza tija kwa maofisa ushirika," alisema.

Alisema kwa mwaka huo pia watanunua pikipiki 50 na kompyuta 200 zitanunuliwa na kuanza matumizi ya Mfumo wa Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

"Kuhamasisha, kuratibu na kusimamia ujenzi na ufufuaji wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao. Kwa mfano, tume inasimamia ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU.

"Pia tutaratibu na kuhamasisha ujenzi wa maghala ya mazao ya kilimo ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha mfumo wa minada ya mazao yanayozalishwa na wananchi," alisema.

# Mamlaka yabuni mbinu kuzuia wizi wa mita za maji mitaani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na wizi na uharibifu wa dira (mita) za maji, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA), imebuni mbinu mpya ya kujenga chemba za kuhifadhia dira za wateja ili kudhibiti tatizo hilo.

Chemba hiyo maalum ina uwezo wa kuchukua zaidi ya dira 10, hivyo kuondokana na kufunga dira kwenye nyumba ya mteja kama ilivyo katika maeneo mengine nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka, Mhandisi Justine Rujomba, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwelekeo wa mamlaka kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema hali hiyo inatarajia kuondoa tatizo la wateja kuchezea mita za maji na kusababisha upotevu wa maji ambao umekuwa ukiipa hasara mamlaka hiyo.

"Upotevu wa maji kwa mwaka uliopita ulikuwa asilimia 40 na sasa umepungua hadi asilimia 32. Tunaendelea kudhibiti hii hali lengo ni kufikia chini ya asilimia hiyo. Hizi mita za maji tunazoweka kwenye chemba tunazifungia vizuri na si rahisi mtu kufungua na kuchezea, tunaweka ndani zaidi ya mita 10.

"Mteja yeye anapata maji anatumia na analetewa ankara yake na kabla ya kupatiwa Ankara, msoma mita anapokwenda kufungua kusoma mita anatuma ujumbe unaootesha mita yako yenye namba fulani matumizi ya maji kwa mwezi huo ni uniti kadhaa na kabla ya kutolewa ankra kama una mashaka namba imewekwa pale unapiga na kupewa maelezo au kwenda kujiridhisha," alisema.

Aidha, alisema hadi sasa watu 55 wamekamatwa kwa wizi wa maji na faini ya Sh. milioni 65 zimelipwa.

Hata hivyo, alisema tatizo lingine ambalo linakabili mamlaka hiyo ni wizi wa vyuma chakavu ambapo wamejipanga kutoa elimu kwa kina juu ya utunzaji wa miundombinu hiyo.

Kuhusu mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa Arusha, mkurugenzi huyo alisema utakapokamilika utaongeza upatikanaji wa majisafi kutoka asilimia 75 ya sasa hadi 100 kwa wakazi wa jiji hilo kwa mwaka 2023.

Alisema mradi huo una uwezo wa kuzalisha lita milioni 200 za maji kwa siku huku mahitaji ni lita milioni 124.78 kwa siku.

Pia alisema kupitia mradi wa maji uliopo Hai mkoani Kilimanjaro utasaidia kupeleka huduma hiyo kwenye eneo la Mererani ambalo maji yake yalikuwa hayafai kwa matumizi ya binadamu kutokana na kuwa na madini mengi ya chloride.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha (AUWASA), Mhandisi Justine Rujomba, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio na mwelekeo wa mamlaka hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima wafundwa matumizi mitandao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKULIMA wamesisitizwa kutumia fursa zinazopatikana kwenye mitandao ili kupata taarifa sahihi zitakazowasaidia kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao na kupata masoko.

Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati, Boniface Shoo, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya Nanenane jijini hapo.

"Katika anga la mtandao tunazo fursa nyingi sana zinazowezesha wakulima hasa wa mkoa wetu wa Dodoma wanaojishughulisha na kilimo cha zabibu kupata elimu ya kila namna kuhusu kilimo bora, TCRA tunawasisitiza wakulima kutembelea majukwaa ya kimtandao kupata elimu hii muhimu.

"Pia kubwa zaidi ni kupata mwanga wa mwenendo wa masoko ya bidhaa za mazao yao hasa zabibu," alisisitiza Shoo.

Naye Ofisa Mawasiliano wa TCRA, Robin Ulikaye, alibainisha kuwa wanalenga kuhakikisha wananchi wanapata uelewa na kuepuka matukio ya utapeli kwenye mtandao na wakati wote wanapotumia mawasiliano. "Mtumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu mara anapopokea ujumbe wa kitapeli au kupigiwa simu ya kitapeli kwenye mtandao wake wa mawasiliano, tunamshauri atoe taarifa juu ya utapeli huo kwa kutuma neno 'utapeli' kwenda namba 15040 kisha atapokea ujumbe unaomtaka kuwasilisha namba iliyomtumia ujumbe wa kitapeli; awasilishe namba hiyo na kikosikazi maalum kitapokea taarifa hiyo na kuifanyia kazi," alisema Ulikaye.

Ofisa huyo alisisitiza kuwa kutoa taarifa za utapeli hasa kwa jumbe za "ile pesa tuma kwenye namba hii..." kunasaidia kupunguza matukio ya utapeli mtandaoni.

Pia aliwasisitiza wananchi kutumia huduma za Mawasiliano ya simu kuhakiki namba zao za simu zilizosajiliwa kwa namba za kitambulisho cha taifa ili kuwa salama.

"Uhakiki wa laini za simu zilizosajiliwa kwa kitambulisho chako ni muhimu kwani unaepusha utambulishi wako kutumiwa na mtu mwingine, hasa isivyo halali," alisema.

Kuhusu udhalilishaji mtandaoni, aliwataka wananchi wanaofanyiwa udhalilishaji kwenye mtandao kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili hatua stahiki za kisheria kuchukuliwa.



# Ubalozi wa Ujerumani wasaidia taasisi mil. 226/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UBALOZI wa Ujerumani umetoa zaidi ya Sh. milioni 226 kwa taasisi inayojihusisha na mambo ya Elimu Jumuishi ya Child Support Tanzania (CST), kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu wanaosoma kwenye shule ya taasisi hiyo.

Shule hiyo iliyoko Iwambi jijini hapo, inajumuisha watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali na wasiokuwa na ulemavu wanaohitaji vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidiwa.

Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alitembelea Mkoa wa Mbeya juzi, kabla ya kutembelea kituo hicho na kusaini mkataba wa makubaliano alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kwa ajili ya kujitambulisha.

Baada ya kutembelea kituo hicho kwa ajili ya kuona mazingira ambayo watoto hao wanasomea pamoja na kuongea nao na baada ya kujiridhisha waliingia makubaliano na Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Noela Msuya.

Balozi Regine alisema mradi wao unahusika na masuala ya haki za binadamu na elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu ni sehemu ya utekelezaji wa haki za binadamu.

Alisema waliamua kuisaidia taasisi hiyo kwasababu Mkurugenzi wake ni miongoni mwa watu 15 duniani ambao mwaka 2021 walishinda tuzo ya urafiki ambayo inatolewa na Serikali ya Ujerumani.

"Tumeamua kutoa msaada huu kwa ajili ya kusaidia juhudi za Noela katika kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalumu, elimu ni miongoni mwa haki za watoto hawa kwa hiyo sisi tutaendelea kushirikiana nao," alisema Balozi Regine.

Mkurugenzi wa CST, Noela alisema msaada huo utaisaidia taasisi yake kutekeleza majukumu mbalimbali ya kuwafikia watoto wenye ulemavu na kutoa elimu.

Alisema mradi wanaoutekeleza kwa sasa ni wa miezi mitano nchi nzima kwa kuanzia na Mkoa wa Mbeya ambao wilaya zake zote zitafikiwa.

Alisema taasisi yake inalenga zaidi kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu bila kutengwa na makundi mengine.

"Msaada huu utatusaidia kuondoa pengo lililokuwapo la kuwafikia watoto wenye ulemavu pamoja na kuifikia jamii kwa lengo la kutoa elimu kuhusu haki za kundi hili, kwa hiyo tunaushukuru Ubalozi wa Ujerumani kwa msaada huu," alisema Noela.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Elimu Maalumu Kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambaye ni Ofisa Elimu Maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Wende Mbilinyi, aliishukuru Serikali ya Ujerumani kwa msaada huo.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na kituo hicho kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalumu wanapatiwa elimu na haki zingine kama ilivyo kwa wengine.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, aliupongeza uongozi wa CST kwa kuendelea kutoa elimu jumuishi kwa watoto na kwamba Serikali ya Mkoa itaendelea kushirikiana nao.



Balozi wa Ujerumani hapa nchini, Regine Herse (kushoto), akimkabidhi kadi ya Bima ya Afya mmoja wa watoto wenye mahitaji maalumu wanaosoma katika Kituo cha Child Support Tanzania (CST) cha jijini Mbeya jana, baada ya kutiliana saini na kituo hicho, mkataba wa kutoa msaada wa Sh. milioni 226, kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu. (Wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa CST, Noela Msuya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Asilimia 60 chai ya zamani kuondolewa

**Na Renatha Msungu** MBEYA

BODI ya Chai nchini, imeweka mkakati wa kuondoa asilimia 60 ya chai ya zamani hapa nchini kwenda mpya ili waweze kuongeza uzalishaji wa zao hilo ikiwamo kuongeza mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai nchini, Nicholaus Mauya, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale.

Mauya alisema moja ya mikakati walioweka tasnia hiyo ni pamoja na kubadili mfumo wa kilimo hicho ili wakulima waondokane na mazoea na badala yake watumie teknolojia mpya ya uzalishaji wa zao la chai ili kupanua wigo wa soko la zao hilo hapa nchini.

Alisema wananchi wanapaswa kuendelea kutumia chai ya Tanzania ili kusaidia kupanua wigo wa soko la zao hilo ndani na nje ya nchi ikiwamo wenyewe kujiinua kiuchumi na taifa kwa ujumla.

Vile vile, jamii inapaswa kujenga mazoea ya kutumia chai ya Tanzania kama moja ya kutangaza bidhaa zao, pia watachangia kwa kiasi kikubwa kuiongezea mnyororo wa thamani.

Alisema katika maonyesho hayo Bodi ya Chai wamekuja kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha wanajua na kutambua umuhimu wa chai inayozalishwa nchini pamoja na matumizi yake kwa ujumla. "Naomba wakulima waendelee kutumia chai ya Tanzania wakifanya hivyo watasaidia kupanua wigo wa soko la bidhaa hiyo hapa ndani na nje," alisema Mauya.

Alisema mwelekeo wa tasnia ya chai hivi sasa ni pamoja na kuangalia ubora ili waweze kuzalisha vizuri, kubadili mfumo, kuongeza pembejeo pamoja na idadi ya uzalishaji.

Alifafanua kuwa wanafanya hivyo ili kuongeza uzalishaji wa chai nchini ikiwamo kuhakikisha tasnia ya chai inakuwa kwa kasi nchini hasa ikizingatiwa serikali imeongeza bajeti kwenye sekta ya kilimo.

Alisema wamejipanga kuzalisha chai zaidi ya miche milioni 60 ikiwamo kuongeza uchangiaji wa Pato la Taifa.

Hata hivyo, aliwasisitiza Watanzania kuendelea kununua chai ya Tanzania ili kuiongezea thamani.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa chai Tanzania (TSHTDA), Theophord Ndunguru, alisema moja ya mikakati waliojiwekea kama tasnia ni kuhakikisha wakulima wanatambua mbinu mbalimbali zilizoboreshwa kwenye tasnia hiyo ili waweze kuendeleza kilimo cha kisasa.

Alisema zao la chai ni muhimu wakulima wanapaswa kujua teknolojia ya kisasa ya kilimo chake.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utafiti wa Taasisi ya Chai Tanzania, Dk. Daniel Mgori, alisema ili kuongeza uzalishaji wa chai tasnia hiyo imezingatia utafiti wa aina za chai inayotakiwa kupandwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema watafiti tayari wamegundua aina nane za miche ya chai inayotakiwa kupandwa ili wakulima wavune kwa wingi.

# TARI kutokomeza utapiamlo kupitia mbegu viini lishe

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

WAKATI Tanzania ikiwa mojawapo ya nchi za Afrika inayokabiliwa na utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano kwenye mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Uyole iliyoko mkoani Mbeya imesema ipo tayari kusaidia kumaliza tatizo hilo kwa kutumia mbegu zenye viini lishe.

Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha TARI-Uyole, Dk. Dennis Tippe, akizungumza katika banda ya maonesho ya taasisi hiyo mjini Mbeya alisema suluhisho la utapiamlo linaweza kumalizwa kwa kutumia vyakula vyenye virutubisho vinavyopatikana katika zao la ulezi na mazao mengine kama maharagwe aina ya Jesca yanayozalishwa katika kituo hicho.

Dk. Tippe ambaye ni Mtafiti Mwandamizi wa zao la ulezi taifa, alisema utafiti wa zao hilo uliofanywa na kituo hicho cha Uyole umebaini aina tatu za mbegu mpya kati ya tano walizogundua ikiwamo ya Tari –Fm1, U-15 na P-224 zina virutubisho vya kutosha kwa ajili ya kumaliza tatizo la utapiamlo endapo zitatumiwa kwenye chakula, uji na vinywaji laini.

"Nataka niwafahamishe tu Watanzania faida ya zao hili, ulezi ni moja ya mazao yenye kiwango kikubwa cha nyuzinyuzi kama asilimia 20, ina kiwango kikubwa cha Cabohydrates kama asilimia 65, pamoja na asilimia nane ya protini ambazo zinasaidia sana kwenye magonjwa ya utapiamlo na kisukari," alisema Dk. Tippe.

Alisema tatizo la kuwapo kwa utapiamlo hasa kwenye mikoa inayozalisha chakula linatokana na kuwapo kwa mfumo wa kubadilisha vyakula na kuachana na vyakula vya asili ikiwamo ulezi ambao umekuwa na virutubisho vingi kwa ajili ya mwili wa binadamu.

Alisema kutokana na umuhimu wa zao hilo kituo cha Uyole kimeshafanya utafiti aina za mbegu za asili 16 za mazao ya ulezi kwa kuchukua vinasaba kwa kuwa mazao hayo katika siku za hivi karibuni yalisahaulika katika kilimo kutokana na mahitaji ya soko.

Dk. Tippe alisema, ulezi ukitumika kama chakula una uwezo mkubwa wa kukaa muda mrefu bila kusagika na kuleta virutubisho vya kutosha kwa maisha ya binadamu katika kupambana na magonjwa mbalimbali. Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema matokeo ya utafiti wanaofanya ni ugunduzi wa mbegu bora kwenye mazao ya mihogo, maharagwe, mahindi, ulezi na viazi vitamu ambazo zinachangia lishe. Dk. Mkamilo alitolea mfano zao la maharage ipo mbegu aina ya Jesca na Siliani ambazo zina kiwango kikubwa cha madini ya chuma na zinki na kwenye mahindi ya njano kuna mbegu yenye protini ya kutosha pamoja na viazi lishe vinatoa vitamin A kwa wingi kwa kusaidia wajawazito.

Akizungumzia tatizo la utapiamlo kwenye maeneo ya uzalishaji wa chakula kwa wingi, alisema shida iliyoko watu wanaweza kuwa wanalima kwa wingi, lakini sio walaji wa mazao hayo na badala yake kutumia kwa ajili ya biashara.

"Takwimu zinaonyesha kuwa maeneo ya uzalishaji wa mazao ya chakula ndiyo yenye tatizo la utapiamlo sababu kubwa utakuta mkulima hata kile anachokilima hakitumii kwa ajili ya chakula, jambo linalohitajika hapa sio kuzalisha sana bali ni kula hivyo vyakula sana wanavyovizalisha," alisema Dk. Mkamilo.



# Ugonjwa wa surua waripotiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema imebaini viashiria vya ugonjwa wa surua kutoka katika vituo vya afya vya Unguja na Pemba.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wagonjwa 80 wameripotiwa wakiwamo 65 kutoka Unguja na 15 Pemba.

Mazrui alisema wizara inafuatilia kwa karibu taarifa za uwapo wa ugonjwa huo ili kutoa taarifa kwa wakati kwa wananchi ingawa hadi sasa hakuna kifo kilichoripotiwa kutokana na maradhi hayo.

Aidha, alisema kati ya sampuli 30 zilizokusanywa na kupelekwa maabara ya taifa Tanzania Bara, tatu zimethibitisha ugonjwa huo.

Ugonjwa wa surua, Mazrui alisema ni moja ya maradhi ya kuambukiza ambayo husababishwa na virusi aina ya 'Morbillivirus paramyxvirus' vinavyoelea kwa haraka kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya hewa au kugusa majimaji yatokanayo na mwenye maambukizi.

"Ugonjwa huu huambukizwa pale mtu anayepata maambukizo ya vimelea hivi anapokohoa, kupiga chafya au kugusa sehemu zinazotumiwa na watu wengine," alisema.

Hata hivyo, alisema ugonjwa huo huwaathiri watu wa rika zote lakini zaidi ni watoto chini ya umri wa miaka mitano, wajawazito na watu wenye upungufu wa kinga mwilini.

Alizitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni pamoja na homa kali, kukohoa, mafua na macho kuwa mekundu ambayo huambatana na vipele harara ambazo hujitokeza katika paji la uso na hata mwili mzima pamoja na vidonda mdomoni au koo kuuma.

Mazrui aliwaomba wananchi wanaopata dalili hizo kufika vituo vya afya haraka ili kupata matibabu na kuwataka watumishi na wamiliki wa vituo vya afya kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa kuzingatia utekelezaji wa kulinda watumishi na watoa huduma.

Alisema wizara itaendelea kufuatilia mlipuko wa ugonjwa huo kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na washirika wengine wa maendeleo ili kuudhibiti haraka.

Kwa mujibu wa WHO, surua ni mojawapo ya sababu kuu za vifo miongoni mwa watoto wadogo ingawa chanjo salama na ya gharama nafuu inapatikana.

Mwaka 2015, kulikuwa na vifo 134, 200 vya surua duniani, takriban vifo 367 kila siku au vifo 15 kila saa.

Hata hivyo, chanjo ya surua ilisababisha kupungua kwa asilimia 79 kwa vifo vya ugonjwa huo kati ya mwaka 2000 na 2015 duniani kote.

Mwaka wa 2015, takriban asilimia ya watoto duniani walipokea dozi moja ya chanjo ya surua katika siku yao ya kwanza ya kuzaliwa kupitia huduma za kawaida za afya kutoka asilimia 73 mwaka 2000 na mwaka 2000-2015 chanjo ya surua ilizuia takriban vifo milioni 20.3.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akishuhudia Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame (kulia) na Waziri wa Nishati wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, January Makamba, wakitiliana saini na makabidhiano ya data za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwenye vitalu vya Zanzibar, Ikulu Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri awahimiza wananchi kilimo hai

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, amewaomba wananchi wakiwamo wakulima kujikita katika kilimo hai ili kupata uhakika wa chakula.

Akizungumza jana wakati alipotembelea banda linalotoa elimu kuhusiana na kilimo hai katika maonesho ya Nanenane Kizimbani.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kilimo hai ni muhimu kwa wakulima na kitawasaidia kupunguza gharama za pembejeo.

Alisema miongoni mwa faida za kilimo hicho ni kuwa na uhakika wa soko la bidhaa zinazozalishwa ambapo mbolea za asili zinasaidia kuimarisha ardhi.

Pia aliwahimiza wananchi kufika katika banda hilo kupatiwa elimu na wataalamu waliopo ikiwamo jinsi ya kutengeneza mbolea kwa kutumia taka na wadudu.

Ofisa kutoka Milele Zanzibar Foundation, Alice Mushi, alisema lengo lao ni kuwadhihirishia wakulima wa Zanzibar kuwa kilimo hai kinawezekana na kina tija.

Mratibu wa Kituo cha Stone Town, Nuru Mtema, alisema lengo ni kuona jamii inalima kilimo hai na kwamba kilimo hicho kinazingatia uhalisia wa kilimo na kulinda afya ya walaji.

**Alisema miongoni mwa faida za kilimo hicho ni kuwa na uhakika wa soko la bidhaa zinazozalishwa ambapo mbolea za asili zinasaidia kuimarisha ardhi.**

# DC mpya awaomba wananchi ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Yussuf Mkasaba, amesisitiza ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake kwa azma ya kuwatumikia wananchi ipasavyo na hatimaye kufikia lengo lililokusudiwa.

Hayo aliyasema jana ofisini kwake, Makunduchi baada ya makabidhiano ya ofisi yaliyofanyika kati yake na aliyekuwa Kaimu Mkuu wa Wilaya hiyo, Marina Joel Thomas, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kati katika mkoa huo.

Mkuu huyo mpya wa Wilaya alisema ushirikiano ndio msingi mkubwa wa utendaji kazi na bila ya kuwapo ushirikiano hakuna maendeleo yatakayofikiwa.

Alisema ni matarajio yake kwamba kuwapo mashirikiano kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendaji wa kazi hasa kwa umuhimu wa ofisi hiyo sambamba na kwenda na kasi ya maendeleo iliyokusudiwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Pia alisema mbali na uwapo ushirikiano, suala la kuimarisha amani, umoja, utulivu na mshikamano ni la lazima katika wilaya hiyo kwa lengo la kuwatumikia wananchi.

Sambamba na hayo, alisema ushirikiano utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Rais Dk. Mwinyi ana maono makubwa katika kuwapelekea wananchi wake maendeleo, hivyo ushirikiano wa pamoja utasaidia katika kufikia lengo hilo," alisema Mkasaba.

Mkuu wa Wilaya ya Kati, Thomas, aliwataka viongozi na watendaji wote wa wilaya hiyo kumpa ushirikiano mkubwa ili iwe rahisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mwalimu Said Hamad Ramadhan kwa niaba ya wazee wa wilaya hiyo alimkaribisha mkuu huyo mpya wa wilaya na kumweleza kwamba kwa niaba ya wazee wote wamempokea na wako tayari kufanya kazi naye wakati wote.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAPPINESS HENDRY MINJA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 477 CYC, CHASSIS NAMBA: MD2B15BX2MWB95158, ENGINE NAMBA: JVXWMB40111.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/312512/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**GLADNESS THEOPHILIUS MATANDU** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma vya; kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA: S0248-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MARIAN GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2002,** cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0335-0521** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MZIZIMA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2005,** cheti cha chuo cha **ADVANCED DIPLOMA IN BANKING** chenye usajili namba **IFM/ADB/05/14073** kilichotolewa na **THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT (IFM)** mwaka 2008. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/37692022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 493 ARL, CHASSIS NAMBA: 1C6PCJK28F0002688, ENGINE NAMBA: 156FMIAD2F06320.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/316362/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NSIANDE GABRIEL ULOMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA ALPHARD yenye usajili namba **T264 DPQ ,** CHASSIS NAMBA: **ANH100021429,** ENGINE NAMBA: 2AZ1067157. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**ARU/ARU/RB/315359/2022**

**NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MM/NANSIO - SHAURI LA MADAI Na. 165/2021**

**THEOGENES METHOD RUTECHURA _________MDAI**

**DHIDI YA**

**LETSHEGO TANZANIA. L.T.D ____________ MDAIWA**

**MM/ KISESA - SHAURI LA MADAI NO. 4/2022**

**JACKOBO YOHANA NYANDEKO __________MDAI**

**DHIDI YA**

**BLANDINA ELIAS MWANJALI __________MDAIWA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO NANSIO WILAYA YA UKEREWE - MWANZA NA MAHAKAMA YA MWANZO KISESA WILAYA YA MAGU - MWANZA , TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA , COMPUTER 3 NA PRINTER 2. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA NA.352 KITALU "L" ILIYOPO KISESA MTAA WA ISENI | KISESA MTAA WA ISENI | 14/09/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | COMPUTER 3 | YADI YA NYADHI INVESTMENT – BUSWELU MWANZA. | 25/08/2022 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | PRINTER 2 | YADI YA NYADHI INVESTMENT – BUSWELU MWANZA. | 25/08/2022 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |

116985002

**MASHARTI YA MNADA;**

1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI INAYOHAMISHIKA/ISIYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676***

**Kwa Habari Moto-moto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yataka kusitishwa machafuko mashariki DRC

**KINSHASA,** DRC

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken amesema nchi yake itaunga mkono juhudi zinazoongozwa na Kenya na Angola kusitisha machafuko mashariki mwa Congo.

Blinken alikutana na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi mjini Kinshasa juzi wakati alipofanya ziara.

Mkutano huo uliwajumuisha maofisa wengine wa serikali, akiwemo waziri wa mambo ya kigeni Christophe Lutundula.

Waziri huyo alitoa wito kwa waasi wa M23 na makundi mengi yenye silaha kusitisha uasi wao na kujiunga katika mchakato wa mazungumzo ya amani.

Ziara ya Blinken ilikuwa ya siku mbili na anatarajiwa kuhimiza upatikanaji wa suluhisho la kusitisha machafuko mashariki mwa Congo ambako mashambulizi yameongezeka katika miezi ya karibuni.

DRC inaituhumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 tuhuma ambazo zinakanushwa. Blinken alitarajiwa kuwasili leo nchini Rwanda kukutana na Rais Paul Kagame na Waziri wa Mambo ya kigeni wa nchi hiyo. **DW**

# Wanajeshi wa Israel waua wanamgambo

**TEL AVIV,** ISRAEL

VIKOSI vya Israel vimewaua wanamgambo watatu wa Kipalestina na kuwajeruhi wengine kadhaa katika majibizano ya risasi yaliyozuka wakati wa msako kwenye mji wa Nablus katika eneo linalokaliwa la Ukingo wa Magharibi.

Msako huo ulifanyika juzi siku moja baada ya kufikiwa makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyokomesha machafuko ya siku tatu baina ya Israel na wapiganaji wa Kipalestina wa kundi la Islamic Jihad.

Katika tukio jingine tofauti kwenye mji wa Hebron katika Ukingo wa Magharibi, wizara ya afya ya Palestina ilisema kwamba kijana wa miaka 17 aliuawa kwa risasi na vikosi vya Israel.

Polisi wa Israel, ilisema katika taarifa yake kuwa maofisa wa usalama waliyazingira makazi ya Ibrahim al-Nabulsi, ambaye wanadai alikuwa akitafutwa kwa mfululizo wa mashambulizi ya risasi mapema mwaka huu.



Wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi Kenya wakiendelea na uhesabuji wa kura. **PICHA: MTANDAO.**

# Bomas kuanza mchakato wa kutangaza rais mpya

**NAIROBI,** KENYA

MAOFISA wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) wameanza shughuli ya kusafirisha masanduku ya kupigia kura kwenda katika kituo cha Taifa cha kujumlisha kura cha Bomas mjini Nairobi.

Ili mshindi wa uchaguzi wa Rais atangazwe, sharti fomu asilia za 34A, zifanyiwe uhakiki na tume kabla ya kumtangaza mshindi.

Takwimu zinaashiria asilimia 64.5 ya wapiga kura wote walishiriki kwenye mchakato wa kuwasaka viongozi wapya.

Kwa mujibu wa tume hiyo, watu wasiopungua milioni 14 kati ya milioni 22 wenye sifa walipiga kura kwenye uchaguzi uliofanyika Jumanne.

Hata hivyo idadi hiyo haijajumlisha wapiga kura waliotambuliwa kwa kutumia daftari asilia kwenye baadhi ya maeneo.

Alasiri ya jana Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Wafula Chebukati, alisisitiza kuwa sharti wapokee fomu zote za 34A zilizo na maelezo ya matokeo kabla ya kumtangaza mshindi wa urais.

Juhudi ya kusafirisha makasha ya kura.

Harakati za maofisa wa IEBC zilifanyika kusafirisha masanduku ya kupigia kura yenye matokeo yaliyo nakiliwa kwenye fomu namba 34A.

Tume hiyo ina muda wa wiki moja kujumlisha na kuhakiki matokeo kulingana na katiba kabla ya kumtangaza mshindi.

Fomu hizo zinatokea vituo 46,000 vya kuhesabia kura nchini kote.

Kwa upande wa uchaguzi Pwani ya Kenya, shirika moja la kiraia linawatolea wito viongozi wa kisiasa na wa Kenya kwa jumla kuvuta subira.

Wajumbe wa Asasi hiyo ya Amani ya Taifa na Upatanishi, waliusisitiza umuhimu wa kuipa tume ya uchaguzi muda kufanya kazi yake bila shinikizo la kujumlisha na kuhakiki matokeo ya uchaguzi.

Tarehe ya mwisho ya kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu ni Agosti 16. **DW**

# Zelensky adai vita itamalizwa baada kukombolewa Crimea

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymr Zelensky, amesema kuwa mzozo kati ya nchi yake na Russia, hautamalizika hadi pale rasi ya Crimea katika Bahari Nyeusi, ambayo ilikwapuliwa itakapokombolewa. Katika hotuba yake ya juzi usiku, Zelensky alisema Crimea ni Ukraine, na nchi yake haitoiacha ibakie mikononi mwa Russia.

Crimea imekuwa chini ya udhibiti wa Russia tangu ilipoinyakua rasi hiyo mwaka wa 2014.

Wakati huo huo, watu 13 wamekufa kufuatia mashambulizi ya usiku katika mkoa wa Dnipropetrovsk katikati mwa Ukraine. Zaidi ya majengo 20 yameharibiwa katika mashambulizi hayo. **DW**

# China yaonya kujitenga Taiwan

**BEIJING,** CHINA

CHINA imeonya kwamba haitavumilia vitendo vyovyote vya kutaka kujitenga kwa kisiwa cha Taiwan na kusisitiza itakichukua kwa nguvu ikiwa itahitajika.

Onyo la China limetolewa kutokana na kukiona kisiwa hicho kipo kwenye himaya yake.

Nchi hiyo inafanya mazoezi makubwa ya kijeshi karibu na kisiwa hicho baada ya kuchochewa na ziara ya Spika wa Bunge la Marekani Nancy Pelosi iliyofanyika hivi karibuni. Ofisi ya China inayohusika na Taiwan ilitoa waraka maalum jana, unaoeleza jinsi inavyodhamiria kukinyakua kisiwa hicho kupitia msururu wa hatua za kiuchumi na shinikizo la kijeshi.

Waraka huo ulisema China iko tayari kutengeneza nafasi kubwa ya kuungana upya, lakini haitaacha nafasi kwa vitendo vya kujitenga kwa njia yoyote ile.

China mara ya mwisho ilitoa waraka wa aina hiyo kuhusu Taiwan mwaka wa 2000. Taarifa za hivi karibuni zimearifu kuwa China imetangaza kumalizika kwa luteka zake kuizunguka Taiwan

**BBC**

# NAMUNGO YASHUSHA BEKI 'NDUGU' WA OKRAH SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo FC imemsajili beki 'ndugu' wa taifa moja, Emmanuel Asante kutoka klabu ya Bechem United ya Ghana aliyotoka kiungo wa Simba, Agustine Okrah.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa, mbali na klabu hiyo, beki huyo wa kati pia amewahi kuitumikia Klabu ya Asante Kotoko ya nchini humo.

"Mlinzi wa kimataifa kutoka Ghana Emmanuel Asante, aliyewahi kuwa Asante Kotoko, Olympics na msimu uliopita akiichezea Bechem United ni 'Muuaji wa Kusini' kwa mkataba wa miaka miwili," iliandika taarifa ya klabu hiyo.

Namungo imemtambulisha mchezaji huyo kutoka Afrika Magharibi, siku moja tu baada ya kumtangaza kiungo kutoka Togo, Seidou Blandja, lakini ikimsajili Christian Oruchum kutoka Tusker ya Kenya.

Wengine iliowasajili kuelekea msimu mpya wa 2022/23, ni Abdul Haji Omar, James Mwashinga, Hassan Kabunda na Pius Buswita.

Namungo imeachana na wachezaji kadhaa wakiwamo Abdulaziz Makame, Sixtus Sabilo, Haruna Shamte, Vicent Philipo, Haruna Shamte na wengineo.

Pazia la Ligi Kuu Bara linatarajiwa kufunguliwa rasmi Agosti 15, mwaka huu kwa kupigwa mechi mbili ambapo Namungo FC itakuwa nyumbani katika Uwanja wa Majaliwa kuikaribisha Mtibwa Sugar huku Ihefu FC ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Dimba la Highland Estate, Mbeya.

## HONGERENI...



Wachezaji wa Timu ya Tanzania iliyoshiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola nchini Uingereza, wakiwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, huku wakipokelewa kwa bashasha na wenza wao, watoto, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na wadau mbalimbali wa michezo nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kipanga yafunguka kuanzia ugenini CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kupangwa kucheza dhidi ya Hilali FC Wau ya Sudan ya Kusini kwenye mechi ya hatua ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa timu ya Kipanga FC, Hassan Abdulrahman, amefurahia kuanzia ugenini huku akieleza kuwa kikubwa ni kuanza maandalizi mapema ili kuweza kufanya vizuri.

Alisema kuanzia ugenini wao wanachukulia kama fursa ili mechi ya marejeano wafanye vizuri katika uwanja wao wa nyumbani.

Akizungumzia juu ya wapinzani wao, alisema wanaendelea kuwafuatilia kwa karibu ikiwamo kuwasoma mbinu zao kama ilivyokawaida kwa mchezo wa mpira wa miguu.

**"Tunaendelea kuwafuatilia kwa ukaribu mkubwa wap inzani wetu Hilali FC WAU, kwa sababu ili tufanye vi zuri lazima tujue mbinu za wapinzani wetu na sisi len go letu ni kufanya vizuri," alisema.**

Hata hivyo, alisema kuwa mipango yao ya kufanya vizuri katika michuano hiyo ya kimataifa ipo palepale na kwamba haijalishi wanakwenda kukutana na nani.

Wawakilishi wengine wa Zanzibar katika michuano ya kimataifa ni mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM, ambao watakuwa na kazi moja tu ya kuipeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo wataanzia hatua ya awali nyumbani dhidi ya Al Ahali Tripoli FC ya Libya.

Mechi hizo zitapigwa kati ya Septemba 9-11 na za marudiano zikichezwa Septemba 16-18, mwaka huu.

# TFF yapiga 'stop' viwanja vitano, yaruhusu tisa

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesimamisha viwanja vitano kutumika kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu kutokana na kutokidhi vigezo, huku vitatu vikitarajiwa kuruhusiwa baada ya marekebisho yanayoendelea kukamilika kabla ya kupitishwa na Kamati ya Leseni za Klabu.

Taarifa iliyotolewa jana na TFF, na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa jumla ya viwanja tisa vimepitishwa kwa ajili ya kutumika kwenye Ligi Kuu msimu wa 2022/23.

Taarifa hiyo ya TFF inakuja wiki chache baada ya kuvitaka viwanja kadhaa kufanyiwa marekebisho kabla ya ligi kuanza, la sivyo havitopitishwa na Kamati ya Leseni za Klabu.

Viwanja vilivyosimamishwa ni Mkwakwani Tanga, Nyankumbu Girls ya Geita, Ushirika Moshi, Mabatini Mlandizi mkoani Pwani na Jamhuri Dodoma.

Mkwakwani hutumika na Coastal Union kama uwanja wa nyumbani, Nyankumbu msimu uliopita ulikuwa ni uwanja uliotumiwa na Geita Gold, Ushirika ukitumiwa na Polisi Tanzania, Mabatini Pwani hutumiwa na Ruvu Shooting, huku Jamhuri Dodoma ukitumiwa na Dodoma Jiji FC.

Kwa maana hiyo, timu hizo zitalazimika kutafuta viwanja mbadala.

Viwanja ambavyo vipo kwenye marekebisho na vitaruhusiwa baada ya kukamilika ni Majaliwa wa Ruangwa Lindi ambao ni uwanja wa nyumbani wa Namungo, Kaitaba, unaotumiwa na Kagera Sugar na Sokoine Mbeya ambao hutumiwa na timu mbili za Prisons na Mbeya City.

Viwanja tisa ambavyo vimepitishwa kupigiwa kipute ni Benjamin Mkapa, Dar es Salaam vinavyotumiwa na Simba na Yanga, CCM Kirumba, Azam Complex, Chamazi ambao ni uwanja wa nyumbani wa Azam FC, Highland Estate, Mbarali Mbeya utakaotumiwa na Ihefu, Karatu Arusha, Liti Singida utakaotumiwa na Singida Big Stars, Manungu Turiani, Morogoro wa Mtibwa Sugar, Sheikh Amri Abeid, Arusha na Uhuru, Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG NA CHELSEA
CHELSEA pia itaamua wiki hii iwapo itamsajili mshambuliaji wa Barcelona na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33. ***(FourFourTwo)***

### SARR AWINDWA UNITED
BAADA ya kumaliza nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Austria anayecheza Bologna, Marko Arnautovic mwenye umri wa miaka 33, Manchester United sasa itaelekeza mawazo yao kwa mshambuliaji wa Watford raia wa Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 24. (***Sun***)

### ARSENAL YAMGEUKIA TONALI
ARSENAL wanafanya mazungumzo ya kumsajili kiungo wa AC Milan, Sandro Tonali mwenye umri wa miaka 22, lakini wababe hao wa Serie A wanataka pauni milioni 46 kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia. ***(Daily Mail)***

### ATLETICO KUMUUZA MORATA
MANCHESTER United pia wamepewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Hispania na straika wa zamani wa Chelsea, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 29, ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake pale Atletico Madrid. ***(ESPN)***

### CHELSEA KUVUNJA BENKI
CHELSEA inaweza kuwasilisha dau la kuvunja rekodi la pauni milioni 85 kwa mlinzi wa kati wa Leicester City, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21 ambaye anawaniwa pia na Paris St-Germain. ***(talkSPORT)***

### GAKPO NAYE ATAKIWA
MSHAMBULIAJI wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, ni nyota mwingine anayeivutia Manchester United, lakini watalazimika kutoa takriban pauni milioni 35 ili kuinasa saini yake. ***(Telegraph)***

### ARTETA AMTAKA PINO
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta pia yuko tayari kuipiku Liverpool katika mbio za kumsajili kwa pauni milioni 33, winga wa Villarreal, Yeremi Pino mwenye umri wa miaka 19. ***(Metro)***

### TUCHEL KWA CASADEI
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel anaandaa mbinu nyingine ya kumsaka kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 19, huku Inter Milan ikitarajiwa kukubali ada ya pauni milioni 12. ***(Evening Standard)***

### COLLADO AWANIWA BARCA
WINGA wa Barcelona, Alex Collado mwenye umri wa miaka 23, ananyatiwa na mabingwa wa Ligi Kuu Scotland, Celtic. ***(Daily Record)***

### RAMOS AMULIKWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inatarajiwa kuwasilisha ombi la kwanza la kumnunua mshambuliaji wa Benfica, Goncalo Ramos mwenye umri wa miaka 21, ambaye analengwa na klabu ya Paris St-Germain. ***(Daily Express)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN CITY YAPAMBANA VIKALI KUMBAKIZA SILVA

Nyota huyo ameibuka kama shabaha ya Barcelona licha ya matatizo yao ya kifedha...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imemwambia Bernardo Silva kuwa hawataki kumwachia msimu huu wa majira ya joto licha ya juhudi za Barcelona kutaka kumsajili, kwa mujibu wa 90min.

Wawakilishi wa Silva wameiambia Man City kwamba, mchezaji huyo atakuwa tayari kuhamia hapo Camp Nou, lakini mabingwa hao wa Ligi ya England wamesimama kidete na msimamo wao.

Ripoti katika vyombo vya habari vya Katalunya zimependekeza makubaliano yamekubaliwa kati ya klabu hizo mbili, lakini taarifa hizo zimekanushwa na City.

City wameweka wazi kwa Silva kwamba, baada ya kumpa mkataba mpya Machi mwaka huu, hawana nia ya kumuacha aondoke chini ya miezi sita.

Silva aliomba kuondoka majira ya joto yaliyopita wakati ilionekana kwamba hangeweza kuwa na nafasi ya kutosha katika mipango ya kikosi cha kwanza cha Pep Guardiola.

Lakini Silva alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa City walipotwaa taji lingine la Ligi Kuu msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ameibuka kama shabaha ya Barcelona licha ya matatizo yao ya kifedha yanayoendelea.

Huku mustakabali wa Frenki de Jong ukiwa bado haujulikani, lakini imetaarifiwa kwamba, Barcelona wamemwambia Silva hata kama Mholanzi huyo atabakia bado wanataka kumsajili.

Wakuu wa City, Txiki Begiristain na Ferran Soriano, wote waliowahi kuwa wachezaji wa zamani wa Barca, wameweka wazi kwa klabu yao ya zamani kwamba, hawataki kufanya biashara nao kuhusu Silva msimu huu wa majira ya joto, lakini inabaki kuonekana kama miamba hao wa Katalunya watasikiliza maoni yao au la.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,021,2

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 11 NA 12 AGOSTI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/08/22 | 17:00 | Tobol Kostanay vs Zrinjski Mostar | 2.52 | 3.27 | 2.72 |
| 02. 11/08/22 | 19:00 | Chojnice vs ZKS Stal Rzeszow | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 11/08/22 | 19:30 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.29 | 2.82 | 3.52 |
| 04. 11/08/22 | 20:30 | Panathinaikos vs Slavia Prague | 2.44 | 3.13 | 2.93 |
| 05. 11/08/22 | 21:00 | KI Klaksvik vs KF Ballkani | 2.23 | 3.38 | 3.08 |
| 06. 11/08/22 | 21:00 | Shkendija vs AIK Football | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 07. 11/08/22 | 21:00 | Hibernians vs Rigas Futbola Skola | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 08. 11/08/22 | 22:00 | West Bromwich vs Sheffield Utd | 2.24 | 3.26 | 3.11 |
| 09. 12/08/22 | 01:00 | Mvo Wanderers vs CA Fenix | 2.28 | 3.17 | 3.17 |
| 10. 12/08/22 | 05:00 | Queretaro FC vs San Luis | 2.26 | 3.21 | 3.11 |
| 11. 12/08/22 | 18:30 | IF Gnistan vs FF Jaro | 2.92 | 3.51 | 2.26 |
| 12. 12/08/22 | 19:00 | Miedz Legnica vs Zaglebie Lubin | 2.46 | 3.15 | 2.66 |
| 13. 12/08/22 | 19:30 | Kaiserslautern vs Paderborn | 2.54 | 3.43 | 2.54 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa, vodacom m-pesa, BREAKING, airtel money, ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa


SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WERNER AREJEA RASMI RB LEIPZIG KUTOKA CHELSEA



**LEIPZING, Ujerumani**

KLABU ya RB Leipzig imethibitisha kumsajili kwa mkataba wa kudumu, Timo Werner kutoka Chelsea na amesaini miaka minne.

Mjerumani huyo alihamia upande tofauti miaka miwili iliyopita kwa pauni milioni 47.5, lakini alishindwa kufikia kiwango kilichotarajiwa pale Stamford Bridge, akifunga mabao 23 katika mechi 89 alizoichezea Chelsea na hatimaye kujikuta akikosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Thomas Tuchel.

Mzozo kati ya Tuchel na Werner kutokana na kukosa dakika za kutosha kucheza, ulianza msimu uliopita na ilionekana wazi kwamba ataondoka kurudi Leipzig.

Werner amefuata nyayo za mchezaji mwenzake wa zamani, Romelu Lukaku, akiwaacha Chelsea na Armando Broja, Michy Batshuayi na Kai Havertz kama chaguo la kuongoza mashambulizi ya Tuchel.

The Blues hao tayari wameimarisha safu yao ya ushambuliaji msimu huu wa majira ya joto kwa kumsajili Raheem Sterling kwa pauni milioni 45.

Tuchel pia anatarajia kuongeza safu yake ya mbele kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto kufungwa na anaweza kuidhinisha uhamisho wa Wilfried Zaha wa Crystal Palace, ambaye ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake wa miaka mitano ambayo alisaini mwaka 2018.

Ujio wa Zaha unaweza kuambatana na kuondoka kwa winga chipukizi, Callum Hudson-Odoi, ambaye amekuwa na wasiwasi juu ya nafasi yake chini ya Tuchel na yuko tayari kushinikiza kuondoka Stamford Bridge msimu huu wa majira ya joto.

# Sanchez sasa mali ya Marseille

**PARIS, Ufaransa**

ALEXI Sanchez amemalizana na miamba ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Marseille ambao wamethibitisha kuwa walikuwa na makubaliano ya "kimsingi" na mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal na Manchester United.

Inter ilitangaza kusitisha mkataba wa Sanchez siku ya Jumatatu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile, alikuwa sehemu ya kikosi cha Inter kilichoshinda taji la Serie A msimu wa 2020-21, huku pia akifunga bao la ushindi dakika ya 121 dhidi ya Juventus kwenye Supercoppa Italiana, Januari.

Marseille ilitangaza mpango wa kumsajili Sanchez Jumanne, ikisema



katika taarifa yake: "Olympique de Marseille na Alexis Sanchez wamekubaliana juu ya kuwasili kwa mchezaji huyo kupitia makubaliano ya kimsingi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile aliyecheza mechi 143, ambaye ameshinda mataji 17 katika maisha yake ya soka, alijiunga na timu hiyo jana baada ya kufuzu vipimo vya afya yake.

Sanchez atakuwa mchezaji wa 12 kusajiliwa na klabu hiyo katika dirisha hili la usajili, huku mikataba kadhaa ya muda ya msimu uliopita ikifanywa kuwa ya kudumu, pamoja na nyongeza za zingine akiwamo Jordan Veretout, Jonathan Clauss na uhamisho wa mkopo kwa Nuno Tavares.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alifunga mabao matano pekee katika mechi 27 za Serie A alizoichezea Inter msimu uliopita, ingawa alizoanza ni saba tu kati ya hizo.

Kwa jumla, Sanchez alicheza mechi 109 akiwa na 'Nerazzurri' hao baada ya kuwasili kutoka United mwaka 2019, akifunga mabao 20.

208,577/-

# MINZIRO APIGA HESABU NZITO GEITA GOLD CAF

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amefunguka kuwa watapambana hadi tone la mwisho katika mechi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Hilal Alsahil ya Sudan waliopangwa nao hatua ya awali, ili kuhakikisha wanatinga raundi ya kwanza ya kinyang'anyiro hicho.

Katika droo iliyopangwa juzi jijini Cairo, Misri endapo Geita Gold itakayoanzia ugenini itapata matokeo ya jumla, raundi ya kwanza itakutana na Pyramids FC ya Misri.

Geita itashiriki kwa mara ya kwanza mashindano ya kimataifa ambapo mechi za ya awali itaanzia ugenini kati ya Septemba 9-11 kabla ya kurudiana Septemba 16-18, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Minziro alisema anatarajia kukutana na ugumu katika mchezo huo, lakini atapambana kuhakikisha anafanya vizuri. "Ratiba nimeiona, mashindano yoyote huwa yanakuwa magumu na siwajui wapinzani wangu, hivyo nahitaji kupambana ili kupata matokeo mazuri.

" Ukijipanga vizuri utapata matokeo mazuri na iwapo hautojipanga vema basi hautoweza kufanya vema," alisema Minziro.

Timu nyingine yenye dhamana ya kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa upande wa Tanzania Bara ni Azam FC ambayo itaanzia raundi ya kwanza ikisuribi kukutana na mshindi wa jumla kati ya Al Akhder ya Libya dhidi ya Al Ahli Khartoum ya Sudan.

**NEMBO...**




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea zawadi ya nembo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika (CAF), kutoka kwa Rais wa Shirikisho hilo, Dk. Patrice Motsepe, baada ya kufungua Mkutano Mkuu wa 44 wa CAF kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) jana. **PICHA: Ofisi ya Waziri Mkuu**

# Buku tano kuziona Simba SC, Yanga Ngao ya Jamii J'mosi

**Na Joram Gervas, TUDARCo**

KUELEKEA mechi ya Ngao ya Jamii itakayowakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Shirikisho la Soka chini (TFF), limeweka wazi viingilio vya mchezo huo huku kikitaja cha chini kitakuwa Sh. 5,000.

Mchezo huo ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2022/23, unaotarajiwa kuanza rasmi Agosti 15, mwaka huu.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, amesema mechi hiyo inayotarajiwa kupigwa majira ya saa 1:00 usiku huku viingilio vikiwa ni Sh. 30,000 kwa upande wa VIP A, Sh. 20,000 kwa VIP B na Sh. 15,000 kwa VIP C.

Ndimbo alisema alitaja kiingilio kwenye viti vya rangi ya machungwa kuwa ni Sh. 7,000, na Sh 5,000 kwa viti vya rangi ya kijani.

TFF imezitakia klabu zote maandalizi na mchezo mwema kwenye mechi hiyo, ambayo ni lazima mshindi apatikane kwani kama zitakwenda sare, changamoto ya mikwaju ya penalti itachukua nafasi yake.

Msimu uliopita Yanga ilibeba Ngao hiyo baada ya kuifunga Simba bao 1-0 katika mchezo uliopigwa uwanjani hapo, shukrani zikimwendee Fiston Mayele aliyepeleka kilio hicho Msimbazi, Septemba 25, mwaka jana.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/2022 | 17:00 | Brighton vs Newcastle | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 02. 13/08/2022 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.24 | 3.39 | 3.09 |
| 03. 13/08/2022 | 17:00 | Wolverhampton vs Fulham | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 04. 13/08/2022 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 13/08/2022 | 17:00 | Sunderland vs QPR | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 06. 13/08/2022 | 17:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.28 | 2.98 |
| 07. 13/08/2022 | 21:45 | AC Monza Brianz vs Torino | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 08. 14/08/2022 | 13:15 | FC Volendam vs NEC Nijmegen | 2.53 | 3.47 | 2.63 |
| 09. 14/08/2022 | 15:00 | Viborg FF vs Silkeborg IF | 2.83 | 3.48 | 2.36 |
| 10. 14/08/2022 | 16:00 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 11. 14/08/2022 | 16:00 | Troyes vs Toulouse | 2.58 | 3.17 | 2.73 |
| 12. 14/08/2022 | 16:00 | AJ Auxerre vs Angers | 2.28 | 3.11 | 3.21 |
| 13. 14/08/2022 | 16:30 | Mainz vs Union Berlin | 2.29 | 3.26 | 3.06 |
| 14. 14/08/2022 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 15. 14/08/2022 | 18:05 | Nice vs Strasbourg | 2.23 | 3.21 | 3.21 |
| 16. 14/08/2022 | 18:30 | Chelsea vs Tottenham | 2.22 | 3.33 | 3.18 |
| 17. 14/08/2022 | 18:30 | Cadiz CF vs Real Sociedad | 3.13 | 3.13 | 2.35 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 11 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3182 | Hebei Zhongji vs Tianjin Teda | 7.66 | 4.52 | 1.34 |
| 16:30 | 3127 | FK Kyzylzhar Petropavlovsk vs Apoel Nicosia | 4.55 | 3.59 | 1.75 |
| 17:00 | 2127 | FC Olimpik vs Kokand 1912 | 3.58 | 3.04 | 2.03 |
| 17:00 | 3963 | Tobol Kostanay vs Zrinjski Mostar | 2.47 | 3.28 | 2.78 |
| 17:00 | 5122 | Dinamo Samarqand vs Sogdiyona Jizzax | 5.11 | 3.20 | 1.69 |
| 17:30 | 3288 | Al Ahli Doha SC vs Lekhwiya SC | 5.92 | 4.94 | 1.37 |
| 18:00 | 1026 | Hussein Irbid vs FC Maan | 1.41 | 4.05 | 6.91 |
| 18:00 | 5211 | Navbahor Namangan vs Surkhon Termez | 1.42 | 4.03 | 6.88 |
| 19:00 | 1874 | Rakow Czestochowa vs Spartak Trnava | 1.64 | 3.88 | 4.93 |
| 19:00 | 2319 | Viimsi JK vs FC Nomme United | 2.98 | 3.68 | 2.16 |
| 19:00 | 3384 | Nieciecza KS vs Chrobry Glogow | 1.69 | 3.63 | 4.32 |
| 19:00 | 4257 | Hillerod vs HB Koge | 4.72 | 3.84 | 1.59 |
| 19:00 | 5169 | HJK Helsinki vs Maribor | 2.02 | 3.38 | 3.58 |
| 19:00 | 5333 | Ararat Yerevan vs Ararat Armenia | 3.20 | 3.00 | 2.30 |
| 19:30 | 4907 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.18 | 2.87 | 3.72 |
| 19:40 | 4008 | Al Arabi Doha SC vs Al Rayyan SC | 1.91 | 3.40 | 3.54 |
| 20:00 | 1053 | Hapoel Beer Sheva vs FC Lugano | 2.08 | 3.38 | 3.43 |
| 20:00 | 1466 | Twente vs Cukaricki St | 1.28 | 5.42 | 9.84 |
| 20:00 | 2759 | Djurgardens IF vs Sepsi Osk | 1.69 | 3.74 | 4.75 |
| 20:00 | 3472 | Konyaspor vs FC Vaduz | 1.21 | 6.07 | 12.15 |
| 20:00 | 3509 | CFR Cluj vs Shakhter Soligorsk | 1.54 | 3.94 | 6.06 |
| 20:00 | 3815 | Petrocub vs Videoton FC | 4.13 | 3.62 | 1.81 |
| 20:00 | 3919 | FC Basel vs Brondby | 1.72 | 3.74 | 4.54 |
| 20:00 | 4861 | Slovacko vs Fenerbahce | 3.18 | 3.43 | 2.16 |
| 20:00 | 4982 | FC Zurich vs Linfield Belfast | 1.23 | 6.04 | 11.07 |
| 20:30 | 1109 | Universitatea Craiova vs Zorya Lugansk | 1.90 | 3.49 | 3.89 |
| 20:30 | 2369 | Royal Antwerp vs Lillestrom | 1.71 | 3.79 | 4.54 |
| 20:30 | 2553 | Panathinaikos vs Slavia Prague | 2.38 | 3.18 | 2.98 |
| 20:30 | 2631 | Steaua Bucuresti vs Dunajska Streda | 1.75 | 3.74 | 4.34 |
| 20:30 | 4021 | KP Polonia Warsaw vs Znicz Pruszkow | 1.99 | 3.29 | 3.39 |
| 20:45 | 3849 | Basaksehir vs Breidablik | 1.22 | 6.04 | 12.07 |
| 21:00 | 2499 | Hibernians vs Rigas Futbola Skola | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 21:00 | 2734 | Levski Sofia vs Hamrun Spartans | 1.27 | 5.44 | 10.08 |
| 21:00 | 2752 | KI Klaksvik vs KF Ballkani | 2.23 | 3.38 | 3.08 |
| 21:00 | 3116 | Anderlecht vs Paide Linnameeskond | 1.06 | 10.07 | 40.28 |
| 21:00 | 3692 | Shkendija vs AIK Football | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 21:00 | 3753 | Dudelange vs Malmo | 5.26 | 4.14 | 1.57 |
| 21:00 | 4275 | Sligo Rovers vs Viking | 4.34 | 3.74 | 1.75 |
| 21:00 | 4858 | Aris Salonica vs Maccabi Tel Aviv | 2.03 | 3.39 | 3.54 |
| 21:30 | 3132 | Lech Poznan vs Vikingur Reykjavik | 1.32 | 5.06 | 8.91 |
| 21:30 | 3135 | Slovan Bratislava vs Olympiakos | 2.98 | 3.13 | 2.41 |
| 21:30 | 4585 | Ruch Chorzow vs Gornik Leczna | 2.11 | 3.19 | 3.19 |
| 21:30 | 5532 | Rapid Vienna vs Neftchi Baku | 1.42 | 4.56 | 6.89 |
| 21:45 | 4595 | St Patricks vs CSKA Sofia | 3.48 | 3.28 | 2.10 |
| 22:00 | 1088 | BSC Young Boys vs KuPS Kuopio | 1.15 | 7.06 | 17.14 |
| 22:00 | 1632 | Partizan vs AEK Larnaca | 1.65 | 3.93 | 4.74 |
| 22:00 | 1961 | Kisvarda FC vs Molde | 4.44 | 3.68 | 1.75 |
| 22:00 | 2165 | AZ Alkmaar vs Dundee Utd | 1.21 | 5.87 | 13.15 |
| 22:00 | 2324 | Gil Vicente vs FC Riga | 1.47 | 4.34 | 6.25 |
| 22:00 | 3165 | West Bromwich vs Sheffield Utd | 2.24 | 3.26 | 3.11 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Agosti 11, 2022

Nipashe






Man City yapambana vikali kumbakiza Silva

MKUTANO CAF...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimsikiliza Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika (CAF), Dk. Patrice Motsepe (kulia), wakati wakiongozana jana kuingia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kufungua Mkutano Mkuu wa 44 wa CAF. (Wa pili kulia) ni Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino na kushoto ni Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa. **Picha: Ofisi ya Waziri Mkuu**

# Bingwa Super Cup kubeba bilioni 233/-

●●● Simba mguu sawa, AFCON nayo yanukia kufanyika Tanzania na Uganda...

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Shirikisho la Soka barani Afrika, Patrice Motsepe, amesema bingwa wa mashindano mapya ya 'CAF Super League, atavuna dola milioni 100 ambayo ni sawa na bilioni 232 za Kitanzania, huku kila timu kati ya 24 zitakazoshiriki kila moja ikipata dola milioni 3.5 sawa na Sh. bilioni nane za Tanzania.

Aidha, kuhusu Tanzania imeelezwa kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa ya AFCON kwa kushirikiana na Uganda.

Akizungumza baada ya Mkutano wa 44 wa CAF uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) , Motsepe, alisema wazo la kuanzisha michuano hiyo limetoka kwa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), Gianni Infantino, ambaye aliongozana naye kwenye mkutano huo.

"Nimshukuru kaka yangu Infantino kwa kutupatia wazo hili ambapo kupitia mashindano haya mapya ya CAF Super League, klabu zitapata fedha nyingi ambapo kwa kuanza kila klabu shiriki itapata dola milioni 3.5 kwa ajili ya kusajili wachezaji, na gharama za michuano kama usafiri na hoteli, lakini timu itakayotwaa ubingwa itapata dola za Marekani milioni 100," alisema Rais huyo wa CAF.

Mpaka sasa CAF haijatangaza timu zitakazoshiriki zaidi ya kutaja idadi ya timu 24 ambazo zinatarajiwa kushiriki ambayo nayo pia yanatarajiwa kucheza kwa makundi.

Hata hivyo, inatarajiwa kuwa CAF itaziteua klabu zitakazoshiriki michuano hiyo kutokana na viwango vya soka ambavyo inavyo kwa sasa na kama ikiwa hivyo Klabu ya Simba inaweza kuwa mojawapo kutokana na kuwa ndani ya 20 bora.

Mbali na hilo kingine kilichojadiliwa ni maendeleo ya soka nchini na Afrika kwa ujumla, ikiwamo ombi la Tanzania kutaka kuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON).

"Tumejadili kuhusiana na maendeleo ya soka, lakini moja kati ya jambo kubwa ni kwamba Tanzania inataka kuwa Mwenyeji wa AFCON wakishirikiana na Uganda, kama unakuwa mwenyeji wa AFCON hii ni michuano mikubwa ya kidunia," alisema Motsepe raia wa Afrika Kusini.

Hilo limeongelewa pia na Rais wa FIFA, Infantino, ambaye alisema kuwa mkutano huo wa Arusha umelenga kuzifanya nchi za Afrika kuwa mwenyeji wa michuano mikubwa ya soka ya kimataifa.

Naye mgeni rasmi wa mkutano huo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, pamoja na mambo mengine alimwomba Rais wa CAF, Motsepe na wanachama wake waliohudhuria mkutano huo kuhudhuria mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga.

Mechi hiyo itachezwa Agosti 13, ikiwa ni ishara ya kuzindua msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23.

## Yanga na Mbrazil, kamati yatajwa

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha imedhamiria kutetea mataji yake kuelekea msimu mpya wa 2023/23, Rais wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said, kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji jana iliunda Kamati Maalum ya Mashindano yenye watu wanane, ikiongozwa na Rodgers Gumbo.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo imewataja wajumbe wanaounda kamati hiyo kuwa ni Mustapha Himba, Lucas Mashauri, Seif Ahmed 'Magari', Pelegrinus Rutayuga, Davis Mosha na Majid Suleiman 'Kaburu'.

Wakati huo huo, klabu ya Singida Big Star imekanusha tetesi zinazoenea kwa kasi kwenye mtandao ya kijamii tangu jana kuwa ina mpango wa kubadilishana winga wao raia wa Brazil, Derio Federico na klabu ya Yanga kwa kuwapa Jesus Moloko.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Singida United, Dismas Ten, amesema hakuna mazungumzo yoyote ya kuuza mchezaji au mabadilishano na klabu yoyote.

"Ninachoweza kusema Derio ni mchezaji wa Singida Big Stars na hivi sasa ninavyokuambia yuko mazoezini na kikosi chake baada ya mechi dhidi ya Mtibwa, tuna mkataba naye wa miaka mitatu na hakuna jambo lolote lililofanyika kuhusu mchezaji huyo kwa sababu huu ni mwanzo tu wa mkataba wake," alisema Ten.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >